





**Mwenyekiti** wa Kijiji, mgambo jela miaka 30 wizi ng'ombe

UKURASA 3




UKURASA 9


# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 18, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581163

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Kikokotoo mafao bado ngoma nzito

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MMOMONYOKO MAADILI WAMSHTUA WAZIRI MKUU

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Tanzania itaendelea kuenzi uhusiano wa kidini na kiutamaduni kati yake na Uganda...

UKURASA WA 5

### SERIKALI YABAINI UPENDELEO ULIPAJI MADENI YA WATUMISHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama amekemea tabia ya baadhi ya waajiri serikalini kutoa ...

# Vurugu zaibuka uchaguzi mdogo, upinzani wajitoa

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Waziri anayeshughulikia Masuala ya Jiji la Kampala, Hajjat Misi Kibanda, juzi alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika maadhimisho ya miaka 75 tangu ulipojengwa msikiti wa kwanza katika Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala. Msikiti huo ulifunguliwa na Mwana wa Mfalme Abdullah wa Zanzibar mwaka 1948. **PICHA: OWM.**

# Muswada wa kuifumua Sheria ya Habari waiva

UKURASA 2

**MICHEZO** NI FAINALI YA KISASI KOMBE LA DUNIA LEO UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na viongozi mbalimbali alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Pemba akiwa na mkewe Maryam Mwinyi (kulia), wakati wa mapokezi kwa ajili ya kuwashukuru Wananchi na wana CCM kisiwani humo kwa kuchaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Taifa wa 10 kushika nafasi hiyo. **PICHA: IKULU**

# Kikokotoo mafao bado ngoma nzito

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimeunda kikosi kazi kwa ajili ya kufuatilia na kushauriana na serikali kuhusu suala la kikokotoo cha mafao.

Hivi karibuni kumekuwapo na madai kuwa CWT inataka kurejeshewa kikokotoo cha awali cha asilimia 50 badala ya asilimia 33 iliyotangazwa na serikali.

Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CWT, Selemani Ikomba, alibainisha kuundwa kwa kikosi kazi hicho juzi baada ya mmoja wa wajumbe wa mkutano huo uliofanyika jijini hapa, kuhoji suala la kikokotoo ambalo bado wanachama wa CWT wapo kwenye sintofahamu.

Ikomba alisema kuwa wakati wa kikao chao cha ndani na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Prof. Joyce Ndalichako, hoja hiyo ilikuwa miongoni mwa zilizowasilishwa.

"Ni kweli ipo task force (kikosi kazi) inaendelea na jambo hilo kwa sababu ukweli ni kwamba lilikubalika na viongozi, na baadhi yetu tulishiriki huko lakini sasa huwezi kusema sikushiriki bali unaweza kwenda kulitafuta, likaja kwa utaratibu mwingine mzuri," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kikosi kazi hicho kinaendelea kufanya kazi na walishirikiana na baadhi ya viongozi kuhusu jambo hilo.

"Kwa hiyo, tutaliweka vizuri ili kufika mahali tunapotaka kufika na Rais wetu Samia Suluhu Hassan ni mwelewa atatusikiliza na ninataka kuamini kuwa atatuelewa kwa njia ya sasa tutakayofuata taratibu," alisema. Sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu liliibuliwa na Nipashe miaka minne iliyopita baada ya kuripoti kwa kina kuhusu kanuni za sheria iliyoanzisha mfuko wa PSSSF baada ya kuunganisha mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF, uamuzi ambao pia uliwezesha nchi kuwa na mifuko miwili ya PSSSF na NSSF.

Kutokana na habari zilizoandikwa mfululizo na gazeti hili kuhusu suala hilo, aliyekuwa Rais kipindi hicho, Hayati Dk. John Magufuli, aliagiza kusitishwa kutumika kwa kanuni za sheria hiyo hadi mwaka 2023, lakini kabla ya kuufikia wakati huo, serikali kwa kushirikiana na wawakilishi wa wafanyakazi walifikia uamuzi wa kuwa na kikokotoo kimoja cha asilimia 33.

Kikokotoo kilichokuwa kimependekezwa awali kwenye kanuni za sheria mpya ya NSSF ambao ni mfuko wa sekta binafsi, ni kuwa mkupuo wa asilimia 25 na mifuko mingine ya watumishi wa umma asilimia 50, sasa watumishi wote wanapostaafu wanapata mkupuo unaofanana wa asilimia 33.

Katika hatua nyingine, mkutano huo ulitoa azimio la kumvua nafasi ya umakamu wa Rais wa CWT, Dinnah Mathamani kutokana na mvutano aliousababisha kwenye mkutano huo kwa kutaka kupindua ajenda ya kujadili masuala ya viongozi.

Mwenyekiti huyo alisema Katiba inataka aitwe mbele ya mkutano asikilizwe lakini hakuwapo kwenye mkutano na alipotafutwa kwa njia ya simu hakupatikana.

"Mkutano ulitoa nafasi ya Mathamani aje kujitetea lakini hajapatikana na kutokana na mkutano huu mwisho leo (juzi), basi utatoa azimio," alisema.

Pamoja na hilo, wajumbe wa mkutano huo waliazimia uitishwe mkutano wa dharura ndani ya miezi mitatu kuanzia juzi ili kujadili kwa kina sababu za wajumbe kumsimamisha Rais wa CWT, Leah Ulaya lakini hao hao pia wamemrudisha.

# Muswada wa kuifumua Sheria ya Habari waiva

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amesema taifa haliwezi kuwa na maendeleo, amani na furaha kama hakuna uhuru wa vyombo vya habari, akisisitiza serikali iko tayari kufanya marekebisho ya sheria.

Amewahakikishia wadau wa sekta ya habari kuwa marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari yanakwenda kufanyika Januari mwakani.

Nape amesema mabadiliko hayo ni safari ya kuwezesha kulindwa kwa uhuru wa habari kwa mujibu wa sheria na siyo utashi wa viongozi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua Kongamano la Kwanza la Maendeleo ya Sekta ya Habari lililoandaliwa na wizara hiyo na kuwakutanisha wadau zaidi ya 1,000 wa sekta hiyo.

Waziri huyo alisema ili taifa liwe na maendeleo, furaha na amani, ni lazima kuwapo kwa uhuru wa habari, hivyo maboresho hayo yanalenga kuimarisha uhuru huo kwa maslahi mapana ya taifa.

"Hakuna furaha, amani na maendeleo kama uhuru wa habari katika jamii hiyo haupo, hivyo ni muhimu kulinda uhuru wa habari ili vitu hivi viwapo kwenye jamii.

"Hilo linawezekana na huo ndiyo msingi wa kongamano hili ambalo linalenga kuleta maendeleo, furaha na msingi wa taifa letu.

"Sheria na kanuni mbalimbali zinaendelea kufanyiwa mabadiliko kwa mujibu wa sheria. Uhuru wa habari unapaswa kulindwa kwa mujibu wa sheria, siyo utashi wa viongozi.

"Kiongozi yeyote atakayekuja atalazimika kuulinda uhuru huu kwa mujibu wa sheria hata kama hataki," alisisitiza Nape.

Waziri huyo alisema kuwa wakati marekebisho ya sheria hiyo yakisubiriwa, uhusiano baina ya sekta ya habari na sekta ya umma umeendelea kuimarika katika uongozi wa serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika kuweka mazingira bora na kutatua kero zinazojitokeza kwenye tasnia ya habari.Alisema sheria na kanuni za habari zinaendelea kufanyiwa marekebisho kwa nia ya kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari kwa mujibu wa sheria.

Nape alisema kuwa baada ya kukutana na wadau na kupokea marekebisho ya baadhi ya vifungu katika Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na kwamba Januari mwakani serikali itakuwa tayari kupeleka marekebisho bungeni ili kuirekebisha sheria.

Alibainisha kuwa nia ya serikali ni kupitia upya sera ya habari nchini na ikiwezekana waunganishe sheria mbili ya habari ya mwaka 2016 na ya utangazaji ili kuwe na sheria moja itakayoshughulikia masuala ya habari.

Pia alisema baada ya sheria hiyo kupitishwa na Bunge, litakuwa jukumu la wadau kwenda kusimamia utekelezaji wake na kuhakikisha waandishi wa habari wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

"Mwaka 2023 tutaweka nguvu za kutosha katika suala la maslahi ya waandishi wa habari na uchumi wa vyombo vya habari, ikiwamo mikataba na ajira ili kuongeza ari katika utendaji wa kazi.

"Pia ni muhimu vyombo vifanye kazi kwa kuzingatia miiko ya nchi yetu, tamaduni na maadili ya uandishi wa habari.

"Serikali inawahakikishia usalama na uhuru katika kutimiza majukumu yenu, niwakumbushe kuwa tuna wajibu wa kulinda nchi yetu, utamaduni wetu, maadili yetu na muhimu sana tuna wajibu wa kulinda rasilimali za nchi hii," alisisitiza.

Nape alitoa angalizo kwa waandishi wa habari kuwa rasilimali za nchi zikitumika vibaya, ni kwa sababu waandishi wa habari wamefumba macho.

"Ni ukweli usiopingika kwamba sekta ya habari ni muhimu sana kwani hata serikali ifanye maendeleo kiasi gani kama wananchi hawapati taarifa ya utekelezaji huo, kwa kweli ni kazi bure.

"Wananchi wasipopata taarifa sahihi na wakati sahihi, inaweza kuwa mwanya wa wapotoshaji kuwaaminisha watanzania kuwa hakuna kinachotekelezwa.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Teknolojia (UNESCO), Mishel Toto, alisema wataendelea kushirikiana na Tanzania kufanya kazi katika kuhamasisha usawa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Jimmy Yonazi alisema wizara hiyo inatambua wajibu wake na matarajio ya watanzania katika kuhakikisha inawapatia waandishi wa habari mazingira mazuri na bora ya upataji habari na kutimiza matarajio ya serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben alisema vyombo vya habari vya kielektroniki vimepiga hatua licha ya kukabiliwa na tatizo la uhaba wa waandishi wa habari wenye kukidhi vigezo vya utangazaji.

"Changamoto nyingine ni mitaala ya ufundishaji haiko katika mfumo wa mafunzo kwa vitendo, waandishi wengi wanatoka vyuoni wakiwa hawajui namna ya kufanya kazi katika vyombo vya habari vya kielektroniki. "Wengi wanatangaza kwa Kiswahili lakini hawakijui vizuri na hatukitamki kama inavyotakiwa," alisema.

Katika kongamano, baadhi ya waandishi wa habari wakongwe waliikosoa serikali kutowatumia waandishi wa habari kwenye matukio muhimu, hasa ziara za viongozi wakuu nje ya nchi.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji wa Mahakama ya Rufaa, Jacobs Mwambegele ametembelea na kukagua zoezi la upigaji wa kura kwenye uchaguzi mdogo wa Jimbo la Amani Tanzania Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Vurugu zaibuka uchaguzi mdogo

**Na Waandishi Wetu,** TANGA

VURUGU zimeibuka wakati upigaji kura ukiendelea katika uchaguzi mdogo wa udiwani wa Mnyanjani jijini Tanga huku vyama vikuu vya upinzani vikijitoa kwenye uchaguzi huo jana.

Kutokana na vurugu hizo, baadhi ya vyama vya upinzani viliamua kuwatoa mawakala wake kwenye vyumba vya kupigia kura huku baadhi ya makada na wafuasi wa vyama vya siasa wakishikana mashati na kupigana, shida hiyo ikiwakumba baadhi ya waandishi wa habari.

Dalili za kutokea vurugu hizo zilionekana kuanzia juzi baada ya wanachama wa ACT Wazalendo kuandamana hadi kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Dk. Spora Liana ambaye ndiye Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo, wakidai kuwa mawakala wao saba kati ya 22 walikuwa wamezuiliwa kushiriki uchaguzi huo licha ya kuapa na kupata vibali vya viapo vyao.

Vyama vilivyotoa mawakala wao kwenye uchaguzi huo mdogo ni Chama cha Wananchi (CUF) na ACT Wazalendo.

Chanzo cha vurugu hizo ni madai kwamba baadhi ya wanachama wa CCM, CUF na ACT Wazalendo waliona masanduku yamejaa kura muda mfupi baada ya kuanza kupiga kura, pia watoto kuonekana kushiriki kupiga kura huku wengine wakidaiwa si wenyeji wa Kata ya Mnyanjani.

Kutokana na madai hayo, wananchi na makada wa vyama hivyo walijazana kwenye nyumba ya mgombea wa CUF na likaibuka kundi la vijana wadogo huku wengine wakishushwa kwenye magari na vurugu zikaibuka huku waandishi wa habari nao wakishambuliwa , wakiwamo wa Nipashe.

Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Tanga, Hamis Mnyeto aliwaambia waandishi wa habari kuwa chama hicho kimejitoa kuendelea na mchakato huo kutokana na vurugu na purukushani nyingi kufanyika mapema jana asubuhi.

"Leo (jana) mawakala wetu walifika kwenye vituo kwa wakati saa 12 kama maelekezo lakini muda wa upigaji kura ulipofika, mawakala wetu walizuiwa na hii ilileta sintofahamu, ndani ya ya muda mfupi tukaona masanduku ya kupigia kura yamejaa wakati hiyo ni saa 1:30 na upigaji kura ulianza saa 1:15 asubuhi.

"Tulifanya uamuzi wa kuwatoa mawakala wetu na tukaondoka nao kwenda kwenye nyumba ya mgombea wetu kwa ajili ya vikao, muda mfupi baadaye wakapita vijana wadogo kwenye eneo ambalo sisi tupo na wananchi wakaanza kuwazomea na baadaye lilikuja kundi la vijana wadogo wakaleta vurugu kwa kuwapiga wanachama wetu.

"Baadhi ya makada wetu walichukuliwa na vijana hao akiwamo aliyekuwa Mbunge wa Tanga, Musa Mbarouk lakini kwa sasa wapo salama Polisi Chumbageni," alisema.

ACT Wazalendo pia walijitoa kushiriki uchaguzi huo kwa madai mawakala wao kuzuiwa kuingia vituoni licha ya kuwa na sifa.

Akitoa msimamo wa chama hicho, Mbarala Maharagande ambaye ni Msimamizi wa uchaguzi wa chama hicho, alisema pamoja na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa kupata ufumbuzi, wasimamizi walishindwa kushughulikia kwa wakati na wameonyesha nia ovu katika uchaguzi huo.

Maharagande alisema chama kimefikia uamuzi wa kuwaondoa mawakala wake wote kwenye vituo vyote 29 vituoni ili kufanya alichokiita "kuwaachia CCM waendelee na uchaguzi wao".

Mgombea Udiwani wa chama hicho, Thobias Haule alisema wananchi na wapigakura wamekosa haki yao ya msingi ya kumchagua kiongozi wao wanayemtaka.

Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Mkoa wa Tanga, Hamad Kidege alisema wapinzani wanapodai tume huru ya uchaguzi, maana yake watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wasiwe waajiriwa wa serikali.

Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi Jimbo la Tanga na Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Dk. Sporah Liana alikiri hali kutokuwa shwari, akifafanua kuwa mchakato ulienda vizuri lakini shida ilitokea pale CUF walipowatoa mawakala wao kwa madai masanduku yamejaa muda mfupi baada ya wananchi kuanza kupiga kura.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe alisema jeshi hilo lilikuwa halimshikilii mtu yeyote kutokana na vurugu hizo.

Alisema CCM Wilaya ya Tanga walilalamikia baadhi ya watu wao kushikiliwa na makada wa CUF.

"Mambo yote yapo vizuri lakini ni kweli CCM wamelalamikia kuwa baadhi ya makada wao walikuwa wanashikiliwa na CUF lakini kwa sasa kila kitu kipo shwari," alisema Kamanda Mwaibambe alipotafutwa na Nipashe jana mchana.

## Mgambo, mwenyekiti wa kijiji jela miaka 30 wizi wa ng'ombe

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

ASKARI wanne wa Jeshi la Akiba (Mgambo) na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Lukala, Kata ya Lukumbule wilayani Tunduru wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya kuhamasisha makundi ya wananchi kwenda kuvamia na kuiba ng'ombe kwa wafugaji wa eneo hilo.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Tunduru, Idran Chuvaka aliyesema mahakama imefikia uamuzi huo baada kujiridhisha na ushahidi ulitolewa na upande wa Jamuhuri na mlalamikaji, Kulwa Tono.

Akitoa adhabu hiyo, Hakimu Chuvaka alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na mashahidi wanne waliletwa na upande wa Jamuhuri kuwa washtakiwa hao walifanya kosa hilo.

Alisema mahakama pia imezingatia maombi yao kwamba iwapatie adhabu ndogo kwa vile hilo ni kosa lao la kwanza, wanategemewa na familia, wazazi na watoto ambao anawasomesha.

Katika shauri hilo la jinai namba 172 la mwaka 2021, waliohukumiwa ni Mohammed Senjele (Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Lukala) aliyedaiwa kuwa chanzo cha tukio hilo, kwamba alipopewa taarifa za kuwapo wafugaji eneo, alikusanya askari wa Jeshi la Akiba na kwenda nao eneo la tukio.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa kiongozi hiyo alipowakuta wafugaji hao, alidai apewe rushwa ya Sh. milioni 10 ili kuwaruhusu kuondoka bila kuwafanya chochote na kwamba baada ya mazungumzo wafugaji hao walidai kutokuwa na kiasi hicho cha fedha, lakini wakakubaliana kumpatia Sh. 500,000.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa baada ya kupewa Sh. 500,000 ambayo ilitumwa kwa njia ya simu ya mwenyekiti huyo ndipo alikwenda pembeni na kusikika akipiga simu kuwa 'wafugaji wenyewe walikuwa wachache tunaweza' na ndipo kundi la watu wengine waliongezeka wakiwa na mapanga na marungu na kuwavamia na kunyang'anya ng'ombe wa wafugaji hao ambao walikimbia na kuwaacha ng'ombe wao kwa kuhofia usalama wao.

Mbali na mwenyekiti huyo, washtakiwa wengine waliohukumiwa ni askari wa Jeshi la Akiba wa kijijini cho waliotambulika kwa majina ya Rashid Lakuu, Mustafa Riziwani, Mustafa Minyand na Halifa Suze, wote wakihukumiwa kwa kupatikana na hatia ya kuhamasisha makundi ya wananchi wa kijiji hicho kwenda kufanya uhalifu wa matukio ya wizi wa ng'ombe 80 kwa wafugaji jamii ya kimang'ati wenye dhamani ya Sh. milioni 64.

Hakimu wakati akisoma hukumu, alisema kitendo kilichofanywa na washtakiwa hao kimemfanya mlalamikaji kushindwa kutimiza majukumu yake ya kuihudumia familia yake.

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka na Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Inspekta Elnest Machia alidai kuwa washtakiwa hao kwa pamoja walitenda kosa hilo Desemba 12 mwaka jana baada ya kwenda kuwavamia wafugaji na kunyang'anya ng'ombe hao kwenye eneo la karibu na kisima nje kidogo ya kijiji hicho ambako walilala wakiwa katika safari ya kuhama kuelekea Kijiji cha Mrusha.



Msaidizi wa Kisheria wa Kituo cha Sauti ya Jamii cha Kipunguni, Dar es Salaam, Tausi Msangi, akitoa mafunzo ya masuala mbalimbali yakiwamo haki na wajibu na aina ya ukatili na madhara yake kwa viongozi wa Kata ya Mzinga. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Mmomonyoko wa maadili washtua

**Na Mwandishi Maalum,** KAMPALA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Tanzania itaendelea kuenzi uhusiano wa kidini na kiutamaduni kati yake na Uganda.

Vilevile, ametoa rai kwa viongozi wa dini kuendelea kukemea mmomonyoko mkubwa wa maadili ambao umeshika hatamu.

Alisema hayo jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika maadhimisho ya miaka 75 tangu ulipojengwa msikiti wa kwanza kwenye Chuo Kikuu cha Makerere kilichoko Kampala, Uganda. Msikiti huo ulifunguliwa na Mwanamfalme Abdullah wa Zanzibar mwaka 1948.

Majaliwa alisema ujenzi wa msikiti huo umekuwa ni chachu ya kuimarisha uhusiano wa enzi kati ya wananchi wa Uganda, Zanzibar na iliyokuwa Tanganyika.

"Nyote mtakubaliana nami kwamba kuwapo kwetu hapa ni ishara tosha ya kutambua umuhimu na mchango wa tukio hili la kihistoria katika kukuza uhusiano wa watu wetu hususan ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Waziri Mkuu aliishukuru Serikali ya Uganda na Chuo Kikuu cha Makerere katika kuusimamia msikiti huo sambamba na kuruhusu Waislamu wa maeneo ya jirani kuutumia kwa ajili ya kuabudu

Katika hatua nyingine, Majaliwa ametoa rai kwa viongozi wa dini kuendelea kukemea mmomonyoko mkubwa wa maadili ambao umeshika hatamu.

"Katika hili ningeomba turejee maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Qur'an tukufu Sura ya 33 Ayah 21 (Quran 33:21) kwamba "Hakika ninyi mnacho kiigizo chema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu".

Aliongeza kuwa taasisi za elimu, jumuiya za dini, viongozi wa dini na viongozi wa umma wanao wajibu wa kuilea jamii kwa kutoa elimu sahihi ya mazingira sambamba na mafundisho sahihi na endelevu ya dini ili kuiwezesha kutambua na kufuata yote yaliyo mema kama ilivyoamrishwa na Mungu na kuacha kabisa yote mabaya yanayomchukiza Mungu.

"Nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wa jumuiya kuongeza juhudi katika kutoa mafunzo ya dini ili kuijengea jamii hofu ya Mwenyezi Mungu dhidi ya maovu na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa mmomonyoko wa maadili tunaoushuhudia sasa," alisema.

Awali akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu

# DC: Rushwa ni tatizo utekelezaji wa miradi

**Na Steven William,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa amesema rushwa ni chanzo cha miradi mingi ya maendeleo yenye manufaa kwa jamii kutokukamilika kwa wakati.

Mohamed Moyo alitoa kauli hiyo jana mjini hapa, akiwakumbusha wadau kupitia mkakati wa kitaifa dhidi ya rushwa, kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema wadau wa maendeleo na taasisi mbalimbali kupitia mkakati wa kitaifa dhidi ya rushwa, wafanye tathmini na kuona namna wanavyoshirikiana katika kutokomeza vitendo vya rushwa nchini.

Katika kongamano la kukuza maadili na vita dhidi ya rushwa mkoani Iringa, Moyo alisema hatua ya kujitathimini mara kwa mara itasaidia kukuza maadili kwenye taasisi mbalimbali pamoja na kukemea na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya rushwa.

Moyo alisema kuwapo kwa vitendo vya rushwa kunaifanya serikali kushindwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuwahudumia wananchi, kwa kuwa baadhi ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hutumika isivyo kutokana na rushwa.

Alisema rushwa ni chanzo cha miradi mingi ya maendeleo yenye manufaa kwa jamii kutokukamilika kwa wakati, akilitumia jukwaa hilo kuwakumbusha wadau kukemea rushwa.

Alisema maadhimisho hayo ni fursa nzuri kwa kila mmoja kujitafakari namna anavyozingatia maadili katika shughuli anazofanya ikiwamo ushiriki wake katika kupinga vitendo vya rushwa kwa kuwa uchumi wa nchi umekuwa ukidumazwa na vitendo hivyo vya rushwa.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamabana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa, Domina Mkama alisema lengo la kongamano hilo ni kuzisaidia taasisi na jamii kufanya kazi bila kutoa au kupokea rushwa.

Aliwahimiza washiriki wa kongamano hilo wakiwamo wawakilishi kutoka klabu za wapinga rushwa vyuoni, kuwahakikisha wanakuwa mabalozi wazuri katika vita dhidi ya rushwa kwa kuielimisha jamii kutambua athari za rushwa kwa maendeleo ya taifa.

# Wizara yahimiza ubora wa bidhaa kuteka soko Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amesema Tanzania itafanikiwa kuingia kwa nguvu kwenye soko la nchi za Afrika ikiwa bidhaa na huduma kutoka nchini zitakuwa zenye ubora wa hali ya juu.

Kigahe alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Kitaifa za Ubora kwa Washindi wa Mwaka 2022 kutoka taasisi na watu binafsi waliofanywa vizuri kwenye masuala ya ubora.

Alisema serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kujenga msingi shindani na endelevu kwa kuweka mazingira shindani na wezeshi kwa wafanyabiashara kwa kuzingatia rasilimali zilizopo nchini, hivyo ni vyema kama taifa kujiweka tayari kuingia kwa nguvu kubwa kwenye soko la nchi za Afrika.

Kigahe alisema nchi za Afrika zinalenga kuboresha biashara baina yake, lakini zimekuwa na kiwango kidogo cha biashara baina yake kulinganishwa na mabara mengine.

Alifafanua kwamba serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliona umuhimu wa kuanzisha tuzo za ubora kitaifa ikiwa ni mpango wake kuboresha huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini kupitia matumizi ya viwango na kanuni za ubora kwa taasisi za umma na sekta binafsi.

Alibainisha kuwa lengo la uamuzi huo ni kuhakikisha mifumo, bidhaa na huduma zinakidhi mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa na hivyo kufanya vizuri kwenye masoko ya ngazi zote.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Athuman Ngenya ambaye shirika lake ndiyo mratibu tuzo hizo, alisema wazalishaji na watoa huduma wote wanahitaji kujengewa au kujijengea utamaduni wa ubora na ushindani nchini na kufahamu uhusiano kati ya ubora na ushindani.

Alisema hiyo ndiyo njia pekee kwa nchi kusonga mbele kibiashara. Alisema tuzo hizo zimefanyika kwa mara ya tatu nchini, serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ikiendelea kujenga mazingira wezeshi kwa kamati inayoratibu tuzo za kitaifa za ubora ili kuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa Dk. Ngenya, tuzo za ubora kwa mwaka 2022 zilikuwa na vipengele vitano, cha kwanza kiliwa tuzo kwa kampuni bora ya mwaka na cha pili ni tuzo kwa bidhaa bora ya mwaka.

Vipengele vingine ni tuzo kwa huduma bora ya mwaka, tuzo kwa muuzaji bora wa bidhaa nje ya nchi na tuzo kwa mtu mmoja aliyefanya vizuri kwenye masuala ya ubora.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama akizungumza na watumishi wa umma katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi wakati wa ziara yake ya kikazi iliyolenga kuhimiza uwajibikaji na kutatua changamoto zinazowakabili watumishi katika halmashauri hiyo.

# Waziri ashtukia upendeleo ulipaji madeni ya watumishi

**Na Mwandishi Wetu,**
IKUNGI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama amekemea tabia ya baadhi ya waajiri serikalini kutoa kipaumbele cha kulipa madeni yasiyo ya mishahara kwa wakuu wa idara pekee na kuyaacha ya watumishi walio wengi, kitendo ambacho kinashusha ari na morali ya utendaji kazi wa watumishi wa umma nchini.

Jenista alikemea tabia hiyo jana wakati wa kikao kazi chake na watumishi wa umma wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida kilicholenga kuhimiza uwajibikaji na kutatua kero zinazowakabili watumishi kwenye halmashauri hiyo.

Alisema kama mwajiri amekusanya mapato na ana lengo la kulipa madeni yasiyotokana na mishahara, anapaswa kutenda haki kwa kuweka usawa katika kulipa madeni ya watumishi na wakuu wa idara badala ya kutoa kipaumbele kwa wakuu wa idara pekee.

"Si haki kwa wakuu wa idara kutengenezewa mkakati wa kulipwa peke yao na watumishi wengine kutolipwa na ikizingatiwa kuwa wanatoa mchango mkubwa katika kuwahudumia wananchi," Jenista alionya.

Waziri huyo aliongeza kuwa kitendo cha waajiri kulipa madeni ya wakuu wa idara pekee, amekikemea mara kwa mara wakati wa vikao kazi vyake na waajiri kwa kuwa kinaathiri saikolojia ya utendaji kazi wa watumishi wa umma na kukwamisha lengo la serikali la kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Waajiri msijali sana maslahi ya wakuu wa idara na kusahau kuzingatia maslahi, haki na stahiki za watumishi wa umma ambao ni wengi kuliko wakuu wa idara, hivyo mnapaswa kuzingatia agizo hili," alisisitiza Jenista.

Akizungumzia madeni ya malimbikizo ya mishahara, Waziri Jenista alisema madeni hayo yamezingatiwa na serikali kwa kuwa tayari Rais Samia Suluhu Hassan ameshaelekeza itengwe fedha, jambo ambalo lilitekelezwa na katika mwaka wa fedha ujao litafanyiwa kazi ili kuendelea kuwalipa watumishi wanaostahili na kuongeza kuwa ofisi yake imejipanga kuhakiki madai yote yatakayowasilishwa ili yalipwe kwa wakati.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alipokea maelekezo ya Waziri Jenista na kuwataka waajiri kuanza kulipa madeni ya watumishi wa umma walio wengi kwa kuwa wakianza kuwalipa wakuu wa idara ambao kila mmoja anadai fedha nyingi, sehemu kubwa ya makusanyo itaishia kulipa madeni ya wakuu wa idara pekee.

"Watumishi walio wengi wanadai kiasi kidogo cha fedha kulinganisha na wakuu wa idara, hivyo wakilipwa hao kwanza, watabakia wakuu wa idara ambao wanadai fedha nyingi, na hata kama wakuu hao wakilipwa mmoja mmoja kiasi chote cha fedha wanachodai wataona thamani ya fedha waliyokuwa wakiidai," alisema Serukamba.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro alimpongeza Rais Samia kwa kuwaletea maendeleo wananchi wa Ikungi, akisisitiza morali ya utendaji kazi kwa watumishi wa umma imeongezeka.

Waziri Jenista Mhagama jana alihitimisha ziara yake ya kikazi mkoani Singida, ikilenga kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma, kutatua kero zinazowakabili watumishi wa umma, kukagua utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

# Mbunge atoa mabati kusaidia ujenzi shule

**Na Neema Hussein**

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Katavi, Martha Marick ametoa msaada wa mabati yenye thamani ya Sh. milioni 2.4 kwa ajili ya ujenzi wa shule ili kuunga mkono mikakati ya serikali katika sekta ya elimu kuhakikisha watoto wanasoma kwenye mazingira bora.

Akizungumza baada ya kukabidhi mabati hayo kwa uongozi wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Katavi, Martha alisema shule hiyo ya Kiislamu itakapokamilika, itatoa elimu kwa wanafunzi wa dini zote ndani ya na nje ya Mkoa wa Katavi.

Aliwaomba wadau wengine kuunga mkono juhudi za viongozi wa Kiislamu mkoani Katavi walioanzisha jambo muhimu la kutanua wigo wa elimu ndani ya mkoa.

Shekh wa Mkoa wa Katavi, Mashaka Kakulukulu alisema matarajio yao ni kuanza kutoa elimu katika misingi ya dini kuanzia darasa la awali mpaka sekondari ili kumjenga mtoto kiimani.

Alisema shule hiyo ambayo imepewa jina la Mufti wa Tanzania, Shekh Abubakar Zuberi, itapokea wanafunzi wa dini zote wa msingi na awali.

Kakulukulu alisema lengo la kuanzisha shule hiyo ni kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika suala la elimu ikiwa ni pamoja na kilio chake kikubwa cha mmomonyoko wa maadili ndani jamii.

Alisema Rais amekua mstari wa mbele kuhakikisha anatetea na kulinda maadili ya mtanzania huku akiwasisitiza kila mara viongozi wa dini kuhakikisha wanawalea watoto kwenye mazingira bora ya kiimani.

Katibu wa BAKWATA Mkoa wa Katavi, Omary Muna alisema lengo lao ni kujenga madarasa 20, nyumba za watumishi tatu, mabweni matatu na zahanati.

Alisema wameanza na ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa kwenye eneo lililotengwa lenye ukubwa wa ekari 9.5.

# Wafugaji wapewa mbinu za ufugaji wenye tija kiuchumi

**Na Julieth Mkireri,**
BAGAMOYO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki amesema ili mifugo iwe na tija ni lazima wafugaji waanze kujifunza kuinenepesha ipate thamani na iwabadilishe kiuchumi.

Ndaki aliyasema hayo jana alipoweka jiwe la msingi la ujenzi wa kiwanda cha nyama na machijio ya kisasa cha Union Meat Abottoirs Limited (UMAL) kilichoko Kwazoka, Kata ya Vigwaza, Halmashauri ya Chalinze wilayani Bagamoyo.

Alisema ni wakati sasa wafugaji kubadilika na kufuga kisasa kwa kuwa na mifugo michache watakayomudu kuihudumia ili iwe na soko kwenye machinjio yanayoanzishwa.

Alisema soko la mifugo kwa sasa limepanda, hivyo ni vyema wafugaji wakajitafakari na kufuga kisasa mifugo michache watakayomudu kuiweka kwenye afya nzuri. "Viwanda hivi ni fursa kwa sisi kupata kipato kwa kuwa bei itaongezeka, hivyo ni vyema kufuga kisasa. Kuwapo kiwanda na machinjio haya ni fursa kwetu kufuga kisasa, tusiendelee kufuga kizamani, hii habari ya kuswaga mifugo kwa masafa marefu inaanza kupitwa na wakati, ng'ombe huyo hatafaa kwa machinjio haya," alisisitiza.

Waziri Ndaki alimpongeza mwekezaji kwa hatua ya kujenga machinjio kwenye eneo hilo ambalo ni sehemu sahihi kutokana na kuzungukwa na idadi kubwa ya wafugaji. Alisema wizara yake imejiandaa kuanza kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa wa tija na maofisa mifugo watawezeshwa kusambaa nchi nzima kutoa elimu. Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete alisema machinjio hayo yanakwenda kutatua kero ya ukosefu wa machinjio kubwa na ya kisasa kwenye halmashauri hiyo.

Alimwomba waziri kusaidia kutatua kero ya baadhi ya wafugaji kugeuza kila eneo kuwa la kulisha mifugo na kuwakumbusha wafugaji kufuga kisasa na kutumia machinjio hayo kujikwamua kiuchumi.

"Tubadilishe mifugo yetu iwe fedha, serikali itengeneze mkakati wa kuona inasaidia wafugaji wenye mifugo mingi lakini pia kuwezesha wawekezaji wa machinjio kama haya yasikose mifugo," alisema.

Alikikumbusha Chama cha Wafugaji kuwaelimisha wafugaji kuwatumia wataalamu kuandaa mifugo yao kwa ajili ya kuifuga kisasa ili ipate soko hususani kwenye machinjio hayo na maeneo mengine.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Kasilda Mgeni alisema mradi huo utakapoanza kufanya kazi, utapanua soko la nyama ndani na nje ya nchi.

Mgeni alisema wilaya hiyo yenye mifugo zaidi ya milion moja, kupitia mradi huo, itachochea ufugaji wa kisasa wenye tija.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Machinjio ya Kisasa UMAL, Mariam Ng'wani alisema mradi huo utakapokamilika, utagharimu Sh. bilion 14 ukiwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 2,000 na mbuzi na kondoo 7,000 kwa siku.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mradi huo unatarajiwa kutoa ajira za kudumu na za muda mfupi 1,500 na wanachi 300 wanatarajiwa kujiajiri kwa kufanya shughuli mbalimba za biashara.

Aliomba wizara kumpatia kitalu kwenye Ranchi ya Ruvu cha hekta 1,000 ambacho kitatumika kupumzishia mifugo ya mradi wa unenepeshaji ili kupata nyama bora itakayoshindana kwenye masoko ya kimataifa.

"Mradi wa unenepeshaji utakwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya kulishia pamoja na ulimaji wa nyasi, pia utatumika kama shamba darasa kwa wafugaji jirani katika kukabiliana na upungufu wa malisho unaowakabili," alisema.

Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama alipongeza kuwapo mradi huo ambao utapunguza kikwazo cha ajira kwenye kata hiyo, pia kutoa fursa kwa wafugaji kujikwamua kiuchumi.

Gama pia aliiomba Wizara ya Mifugo kuona namna ya kuwachimbia malambo kwenye kata hiyo yasaidie wafugaji kupata urahisi wa kunywesha mifugo yao kutokana na kukwazo cha maji kilichopo sasa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, Ngobere Mfamau alisema kuanzishwa kwa mradi huo ni fursa kwa wafugaji na watatoa ushirikiano kwa mwekezaji huo pale watakapohitajika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madudu aliyoyabaini Waziri Mkuu yawape funzo viongozi

**WAZIRI** Mkuu, Kassim Majaliwa, wiki hii alifanya ziara ya kikazi katika mikoa ya Rukwa na Katavi ambako aliibua madudu yaliyofanywa na baadhi ya watendaji katika serikali hasa halmashauri, yakiwamo ubadhirifu wa fedha za umma na miradi ya maendeleo kutekelezwa chini ya kiwango.

Kwa ujumla, ziara hiyo katika mikoa hiyo ambayo kabla ya kugawanywa ulikuwa mmoja, ilionyesha ni namna gani watendaji katika idara na taasisi za serikali walivyojisahau na kufanya makosa ambayo yanawafanya hawa waliowateua kuwa na shaka juu yao.

Akiwa katika manispaa ya Mpanda, alishtuka kusikia kwamba Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA), Hussein Nyemba, ambaye alimwanika hadharani kwamba licha ya kuhamishwa kutoka Igunga kwenda Mpanda, ameendelea na tabia yake ya kutokufuata sheria ya ununuzi. Bila kuuma maneno wala kupepesa macho, Majaliwa alisema kigogo huyo ameongeza kiasi cha fedha kuwalipa waliokuwa wanaidai mamlaka ili ajipatie chochote pamoja na kuharibu mfumo wa malipo kama alivyokuwa akifanya alikokuwa awali.

Licha ya kuongeza kiwango cha madai, alinunua pikipiki kwa bei ya juu kwa nia ya kujipatia fedha kwa kuamua kwenda kununua Dar es Salaam kwa Sh. milioni 3.86 badala ya Sh. milioni 2.7 kwa bei ya Mpanda. Kama vile haitoshi, mkurugenzi huyo alinunua mita 1,000 za maji bila kufuata taratibu za ununuzi pamoja na kushindwa kupeleka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa ajili ya ukaguzi wa ubora.

Licha ya mkurugenzi huyo, Majaliwa aliinyooshea kidole idara ya ardhi katika Manispaa ya Mpanda kutokana na kuwapo kwa migogoro mingi ya ardhi. Aliitaka idara hiyo kujitathmini juu ya utendaji wake.

Katika mkoa wa Rukwa, Waziri Mkuu alielezea kutoridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa miradi ya Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga na Kituo cha Afya cha Matanga wakati serikali imeshatoa zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kazi hizo. Kutokana na hatua hiyo, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuharakisha uchunguzi wa matumizi ya fedha za miradi hiyo.

Akizungumza wakati akikagua ujenzi wa hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga, Waziri Mkuu alisema inashangaza taarifa za ujenzi kuonyesha kuwa kazi imefikia asilimia 91, ikiwa idadi ya majengo yaliyopaswa kujengwa kwa kiasi cha fedha kilichotolewa haijatimia na hakuna miundombinu kama vyoo na mfumo wa maji.


Sambamba na hiyo, Waziri Mkuu aliibua madudu katika ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga baada ya mhasibu na mkufunzi kudaiwa kuchoma nyaraka za mradi huo ili kupoteza ushahidi wa fedha zilizotafunwa.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza TAKUKURU kufanya uchunguzi na kuwahoji wahusika hao ambao wanatuhumiwa kufanya ubadhirifu huo kutokana na kubainika walipoteza ushahidi wa kununua vifaa vya ujenzi mara tatu ya bei inayofahamika.

Kwa ujumla, ziara ya Waziri Mkuu imeonyesha dhahiri kwamba kuna madudu makubwa katika utendaji kazi serikalini hasa katika ngazi ya halmashauri ambako fedha nyingi zinapelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Madudu hayo, kwa mtazamo wetu, kwa kiasi kikubwa yanaonekana wazi kwamba yanatokana na kubebana. Inakuwaje mtu anaharibu sehemu moja na kupelekwa sehemu nyingine huku akiwa na kesi zinazomhusu? Ni vyema serikali ikaliangalia hili kwa namna ya kipekee, vinginevyo fedha za walipakodi zitaendelea kutafunwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wazazi, walezi mngezingatia haya wakati huu wa likizo

**SHULE** za msingi na sekondari tayari zimefungwa, na sasa wanafunzi wako likizo na wanatarajiwa kurudi shuleni Januari mwaka kesho kuendelea na masomo, baada ya kumaliza likizo hiyo ndefu.

Wakati wakiwa shule, ni wazi kwamba wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawakuwa na muda wa kukaa nao au kufuatilia maendeleo ya shule kutokana na kutingwa na shughuli nyingi.

Hizo ndizo huwa ni sababu kubwa za baadhi yao za kushindwa kukaa na watoto wao kujua nini wanakifanya au wanakumbana na vikwazo gani nyumbani, mitaani au shuleni.

Katika mazingira hayo, wanaweza kupata matatizo bila wazazi wenyewe kujua, kutokana na ukweli kwamba hawako karibu nao, hivyo watoto wanaweza kuamua kunyamaza huku wakiumia kwa matatizo wanayokumbana nayo.

Kwa mantiki hiyo si vibaya kipindi hiki cha likizo ambacho watoto au wanafunzi wamerudi nyumbani, wazazi na walezi wakajipa muda wa kuzungumza na watoto wao kila siku.

Watumie likizo hiyo kuwauliza kuhusu vikwazo wanavyokutana navyo wakiwa shuleni, kukagua vitu wanavyovitazama kama picha, simu na vingine, kujadiliana nao kuhusu matokeo yao ya mwaka mzima.

Vilevile wawe makini na aina ya marafiki wanaokuwa nao, na ikiwezekana waangalie historia ya familia za marafiki zao, lakini pia wawape muda wa kwenda kwa wazazi wa pande mbili wajifunze mahusiano na familia.

Pamoja na hayo, si vizuri kuwapa kila wanachotaka, lakini wapewe kwa sababu ni muhimu, lakini pia wasiwadekeze bali wawaruhusu kufanya kazi za mikono bila kujali jinsi, waoshe vyombo, wasafishe nyumba, watandike vitanda vyao, wafue nguo na kazi nyingine za nyumbani.

Wazazi na walezi pia waepuke ugomvi wa mara kwa mara unaoweza kusababisha waathirike kisaikolojia, pia mtoto asishinde chumbani pekee yake akicheza game, awe na muda wa kujichanganya na wengine.

Kujichanganya kwenyewe kuwe na mipaka, kama kuna kazi za kijamii, ikiwamo kutembelea yatima mpe muda afanye hivyo, kwani hatua hiyo inaweza kumfanya awe na tabia ya kujali wengine.

Lakini pia kama ana kipaji, si vibaya kujadiliana naye kuhusu ndoto zake na pia kumweleza hali halisi ya maisha ya sasa ambayo yanaikabili jamii ikiwamo UKIMWI, ushoga na tabia hatarishi.

Ninadhani likizo hii ni nafasi nzuri kwa wazazi na walezi kuwafundisha pia watoto wao unyenyekevu na kuheshimu wengine, kuwatia moyo na kuwajengea uwezo wa kuwa anaweza, badala ya kuwa 'bize'na maisha na kuwaacha wakijiongoza.

Aidha, wakati huu ni wa kujadiliana nao kuhusu hali ya uchumi ilivyo katika familia, ili wajue kuwa katika maisha kuna kupanda na kushuka na pia wafundishwe umuhimu wa kushirikiana na kupeana uzoefu katika matatizo.

Kwa ujumla ni kwamba, ni muhimu kuwa na utaratibu unaoongoza shughuli za mtoto awapo nyumbani, ijulikane kuwa wakati huu wa likizo anapaswa kulala na kuamka saa ngapi na pia muda gani kama wazazi wanaweza kukaa naye na kumpa nafasi ya kuelezea aliyonayo moyoni.

Bila kufanya hivyo, si rahisi kujua mabadiliko ya tabia ya mtoto, hasa wale wanaoishi bweni au wanaotoka nyumbani alfajiri huku wazazi nao wakiwa 'bize' na shughuli zao bila kutenga muda wa kukaa nao.

Ikumbukwe, kipindi hiki cha likizo, ndicho ambacho wanaweza kukitumia kufanya yale ambayo hawakufanya wakiwa shuleni, ikiwamo kuangalia televisheni, kuchati na simu, kulala muda mrefu na mengine ya aina hiyo.

Shuleni huwa wanafunzi wanaongozwa na taratibu, kanuni na sheria za shuleni, lakini wawapo nyumbani, ni vyema wasiachwe huru kupita kiasi na kujikuta wakijiingiza katika makundi yasiyofaa.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kuna maendeleo ya vitu au ya watu miaka 61 ya Uhuru?



Pascal Mayalla

LEO naendelea kudurusu miaka 61 ya uhuru, nikiangazia maadui watatu wakuu tuliokuwa nao tulipopata uhuru. Maadui hao ni ujinga, umaskini na maradhi. Wiki iliyopita nilianza na adui ujinga na leo tunaangazia adui umaskini.

Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alikuwa muumini wa falsafa ya “Maendeleo ya Kweli ni Maendeleo ya Watu na Si Maendeleo ya Vitu”. Falsafa ya uchumi wa serikali ya awamu za Tanzania inabadilika kutokana na Rais wa nchi. Nyerere alikuwa na Ujamaa na Kujitegemea akiongozwa na Azimio la Arusha lenye miiko ya uongozi. Ali Hassan Mwinyi alipoingia akaleta Azimio la Zanzibar, likaondoa miiko ya uongozi. Benjamin Mkapa akaja na sera ya ubinafsishaji, Jakaya Kikwete akaja na soko huria, John Magufuli akaja na kubananisha hadi vyuma vikakaza na sasa Samia Suluhu Hassan kaja, vyuma vimeanza kuachia lakini Watanzania bado ni maskini.

Mama Samia ametoa kipaumbele cha kujenga kwanza uchumi kwa kuendeleza falsafa ya Magufuli ya maendeleo ya vitu kwanza ndipo tuje kwenye maendeleo ya watu ili kulisaidia taifa letu kuja kupata maendeleo ya kweli ambayo ni maendeleo ya watu, baada ya kupata maendeleo ya vitu, ndege, reli na barabara nzuri.

Tanzania ni nchi iliyokuwa ikitegemea kilimo kwa asilimia 80 lakini sasa kutokana na vijana wengi kukimbilia mijini, bado tunategemea kilimo kwa asilimia 67. Kwa maana hiyo, zaidi ya nusu ya Watanzania wanategemea kilimo. Je, kwenye falsafa ya uchumi wa awamu ya tano wamefanya nini kuinua sekta ya kilimo ambayo ndiyo tegemeo kwa uchumi wa walio wengi?

Enzi za Kikwete kuna wakati kilimo kilichangia kupaisha pato la taifa (GDP) ya Tanzania kwa 7.6, lakini ndani ya ukuaji huu wa GDP ya asilimia 7.2, mchango wa kilimo ni asilimia 3.2. japo ukuaji huu ni mdogo, tumshukuru Rais Samia kwa sababu alipoingia, aliikuta sekta ya kilimo iko taabani, akapaisha bajeti ya kilimo kwa zaidi ya mara tatu.

**TUNAHITAJI NINI HASA?**

Hili ni swali la msingi sana, ili taifa letu liendelee. Je, tunahitaji maendeleo gani kwanza? Tuanze kuendeleza watu kwa kuweka mazingira wezeshi ili watu wapate maendeleo, wajenge uchumi imara, wachangie kodi na wachangie uchumi wa taifa ndipo tutumie fedha za ndani kuleta maendeleo ya vitu au tuanze kwa kukopa ili kujenga maendeleo ya vitu kwanza, hata kama ni kwa kukopa, tukishapata vitu, ndipo tuje maendeleo ya watu?

Naomba kutumia falsafa mbili kutolea mifano falsafa ya Mwalimu Nyerere na Falsafa ya Adam Smith. Katika falsafa ya Nyerere, ili tuendelee tunahitaji vitu vinne ambavyo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Watu tunao, ardhi tunayo, siasa safi tunayo? Je, uongozi bora tunao?

Kama vitu hivi vyote vinne tunavyo, Tanzania tumekosa nini? Kwa nini bado ni maskini?. Kati ya watu milioni 61 wa Tanzania, watu milioni 20 wanaishi kwenye lindi la umaskini uliotopea, kwa kipato cha chini ya dola moja kwa siku.

Nyerere alipotangaza Azimio la Arusha la Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, alisema kazi ya kujenga ujamaa ingechukua miaka 30. Lakini siku anatangaza kung’atuka alikiri kuwa tumekosea. Akakiri kwa kusema: “Kufanya kosa si kosa, kosa ni kurudia kosa.”

Je, tulikosea wapi? Tumsikilize mwanauchumi Adam Smith kwenye nadharia yake ambayo itaonyesha kosa la Nyerere. Nadharia ya uchumi ya Adam Smith kuhusu ardhi, mtaji na ujasiriamali,

inashabihiana na nadharia ya Nyerere kwenye watu na ardhi lakini itatofautiana na Nyerere kwenye siasa safi na uongozi bora. Smith anasema tunahitaji mtaji na ujasiriamali, hivyo nadharia ya Nyerere kuweka siasa safi na uongozi bora ni kitu kile kile.

Kwenye nadharia ya Nyerere kulikosekana mtaji. Nyerere alifanya kosa kubwa kwa kuamini fedha si msingi bali ni matokeo. Kiuhalisia, pesa ni msingi sana wa kupata mitaji. Kama una watu, ardhi, una siasa safi na uongozi bora, bila mitaji ya kuwawezesha hao watu kuitumia ardhi kuzalisha mali, tulitwanga maji kwenye kinu kutegemea kilimo cha jembe la mkono kwa kutokuwa na mitaji ya kuchimba madini, mitaji ya kujenga viwanda.

Mwinyi alipoingia, alifanya sera ya ubinafsishaji kuwa fedha za ubinafsishaji zitawekwa kwenye mfuko maalum wa mitaji kuwawezesha Watanzania ili waje kuwa wamiliki wa uchumi wao!. Hapa ndipo matabaka ya wenye nacho na wasio nacho yalipoanzia.

Nadhani ili tusiingizane kwenye mikopo chechefu ya deni la taifa, tufike mahali Tanzania tukitaka kukopa kuingiza kwenye deni la taifa, Bunge lielezwe tunakopa fedha za nini, kiasi gani kwa riba gani ili liidhinishe. Tusije kujikuta taifa linabebeshwa mzigo mkubwa wa madeni.

Japo kuna juhudi mbalimbali zinazofanywa kukabiliana na umaskini uliotopea, ikiwamo mipango au mikakati kama MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA, MKUZA, na TASAF, kuhaulisha familia maskini, lakini bado. Nchi yetu imejaaliwa kila kitu cha kutufanya matajiri. Kwa nini leo miaka 61 ya Uhuru, tukiwa na watu milioni 61, bado ni maskini?, Tunakwama wapi?

**Wasalaam**

**Paskali 0784 270 403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kulikuwa na ulazima kuteketeza vifaranga?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Lakini najiuliza, kulikuwa na haja kweli ya kuwateketeza vifaranga hao huku wakilia kwa uchungu wa kumwagiwa petroli na kisha kuwashwa kiberiti, kweli?**

FIKIRIA uko mahali na jamaa zako mnakula kwa mama lishe, ghafla mwenzako anatafuna mchanga kwenye ubwabwa na badala ya kutema na pengine kushushia kwa maji, anamwaga ubwabwa wote kwa hasira.

Anafanya hivyo huku jirani kuna bibi ombaomba na mwanawe wanasubiri angalau makombo ili nao wapate kitu tumboni na siku ipite. Lakini jamaa anamwaga ubwabwa bila kujali kama kuna watu wenye mahitaji kama hao.

Unafanya nini? Kama mtu mwenye huruma, inakuuma na ikiwezekana basi jichange ili angalau bibi huyo na mwanawe nao wapitishe siku na kitu tumboni, kwa sababu leo unacho kesho huna huenda ikawa zamu yako kusogelea makombo ya wenzio.

Kwa nini nimetolea mfano huu? Bila shaka kuna waliosikia kama mimi, kilichotokea hivi karibuni mkoani Kilimanjaro, ambako vifaranga vya kuku vipatavyo 50,000 viliteketezwa kwa moto kwa kilichoelezwa kuwa ni kukosa soko.

Wateketezaji wa vifaranga hivyo, ni wafanyabiashara wazawa wanaovitotolesha na kuviuza kwa wafuga kuku na wauzaji nyama ya ndege hao, lakini sasa kutokana na ongezeko la uingiaji vifaranga kutoka nje, soko limeadimika.

Wanasema kutokana na ongezeko la vifaranga wageni, hivi sasa hakuna biashara na hivyo wao kutumia fedha nyingi kuvilea, lakini matokeo yake ni kuuza kwa bei ya chini na kukosa faida ya biashara hiyo.

Matokeo yake ni kama mbwai na iwe mbwai, kwa sababu haiwezekani uzalishe kwa gharama kubwa na hatimaye kuja kuuza kwa gharama ndogo, utakuwa ni uendawazimu uliopindukia, bora yaishe kwa kuwateketeza vifaranga hao.

Lakini najiuliza, kulikuwa na haja kweli ya kuwateketeza vifaranga hao huku wakilia kwa uchungu wa kumwagiwa petroli na kisha kuwashwa kiberiti, kweli? Binadamu tunadhani kwa kuwa viumbe wengine hawazungumzi basi hawa wakifanyiwa mateso hawaumii, la hasha, wana hisia kama wewe na wanaumia.

Kwa walioshuhudia ndege wale watoto wakilalamika wakati wakiangamizwa, wajue kuwa kwa dhambi zao siku ya mwisho nao watatokwa machozi kama kuku hao na kuangamia huku wakishuhudia kwa moto wa jehanamu.

Tukio hili linanikumbusha miaka ile vifaranga kama hao walipokamatwa mpakani Arusha baada ya kuingizwa nchini kwa magendo wakitoka nchi jirani ya Kenya na matokeo yake wakateketezwa kwa moto, kana kwamba waliingizwa nchini na shetani. Gumzo hakika lilikuwa kubwa na mijadala kutamalaki.

Juzi kati kuhusu vifaranga hawa, nilimsikia mtaalamu mmoja mtetezi wa wanyama, ambaye bila shaka alipatwa na hisia kama zangu, akisema vifaranga hao hata kama walikuwa na ulazima wa kuteketezwa vile, zingetumia njia zingine za kuwaepusha na maumivu na wakachomwa bila uchungu vile.

Akasema, ingewezekana kabisa wakafungiwa mahali na kisha kupuliziwa hewa ya kaboni daiyoksaidi na wakashikwa na usingizi kama si kupoteza fahamu na kisha kuchomwa kuliko mateso yale waliyopitia.

Hakika kama wangekuwa na uwezo wa kusema kitu, watoto wale wa kuku wangewatazama wale binadamu waliokuwa wakiwamwagia petroli na kuwawasha moto na wangewatamkia: “Enyi binadamu waovu na waonevu, msio na huruma, Mungu anakuoneni kwa jinsi mnavyotuonea kwa makosa yenu wenyewe.”

Hivi kama wale wafugaji vifaranga wangeamua kuwafungulia na kuwaacha huru kila kimoja kijiendee kinakotaka ingekuwaje? Hawaoni wangenufaisha wengine kama ndege mwewe na kunguru au hata wanyama kama paka na mbwa?

Au hata kama si hivyo, je kwa nini wasingewagawa kwenye taasisi za elimu au hata za Jeshi ili zenyewe zingeamua kuwafuga na kufanya watakavyo kuliko kuwaangamiza kwa faida sifuri! Hao ni pamoja na wale waliokamatwa mpakani, kweli suluhisho lilikuwa kuwaangamiza?

Mbona samaki jodari waliokamatwa na Waziri wa Uvuvi enzi hizo, John Magufuli (endelea kupumzika) kutoka mikononi mwa wavuvi haramu wa kichina, waligawiwa kwa taasisi na watu wasio na uwezo na kuchangia kusongesha mbele maisha?

Kulikuwa na sababu gani ya kujichukulia sheria mkononi kana kwamba kama vifaranga wale wangeachwa huru wangesababisha mlipuko wa korona au ebola kwa Watanzania? Siku zingine tuwe tunafikiria kwanza kabla ya kuamua kumwaga ubwabwa kwa sabbu tu umetafuna jiwe, huku kuna wenzio hata punje ya mchele hawana.

**Alamsiki!**

## Jafo apongeza walimu kupokea kampeni ya upandaji wa miti

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo amewapongeza walimu wote nchini kwa kuipokea vizuri na kuitekeleza Kampeni ya Soma na Mti.

Alitoa pongezi hizo juzi alipokaribishwa kuzungumza kwenye Mkutano wa 17 wa Chama cha Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA) uliofanyika jijini Dodoma.

Dk. Jafo alisema kuwa kutokana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi inayoikabili Tanzania na dunia kwa ujumla, wanao wajibu kuendelea kupanda miti ili kukabili athari hizo.

Kampeni hiyo aliyoizindua Januari 20 mwaka huu, inahusisha wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo, ikilenga kuwahamasisha kupanda miti kwa wingi kwenye maeneo yao.

Dk. Jafo alitoa wito kwa walimu hao kuendeleza ajenda ya upandaji miti kwa kuhamasisha pia wazazi wa wanafunzi wao na wananchi kwa ujumla kushiriki katika kampeni ya upandaji miti na usafi wa mazingira.

"Nilipozindua kampeni ya 'Soma na Mti' hapa jijini Dodoma, niliwaomba walimu wote washiriki, na hili nilifanya kwa sababu nchi yetu ina wanafunzi wa shule za msingi na sekondari zaidi milioni 14.1 na wale wa vyuo ni takriban laki nne (400,000), hivyo makisio ya wanafunzi wote ni milioni 14.5, idadi ambayo inaweza kutusaidia kupata miti kwa wingi," alisema.

Hivyo, Waziri Jafo aliwashukuru na kuwapongeza kwa kuipokea vizuri kampeni hiyo huku akiwaomba kuwa mabalozi wazuri kwenye mitaa na vijiji wanakotoka kwa kuhamisha ajenda ya upandaji miti na usafi wa mazingira.

Kuhusu biashara ya kaboni, waziri huyo alisema kwa shule zenye mashamba, mbali na kufaidika na mazao kama vile mikorosho, pia zinaweza kupata fursa ya kuvuna hewa ukaa na kuingiza kipato.



Ofisa wa Benki ya NMB kutoka idara ya uwajibikaji kwa jamii, Aloyce Kikois akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mgama iliyopo Iringa Vijijini walipotembelea shule hiyo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatenga mabilioni kusaidia utekelezaji miradi ya afya, elimu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeendelea kutekeleza uamuzi wake wa kutoa asilimia moja ya faida baada ya kodi, ili kushughulikia mahitaji ya jamii, ikifadhili miradi mbalimbali ya uwekezaji wa kijamii nchini.

Ili kupata matokeo chanya, benki hiyo imeweka vipaumbele katika nguzo kuu tano ambazo ni elimu, afya, mazingira, kilimo na maafa.

Hivi karibuni maofisa kutoka Benki ya NMB walifanya ziara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yenye mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe kufuatilia na kufanya tathmini ya baadhi ya miradi ambayo imefadhiliwa na benki hiyo.

Kwa mujibu wa Meneja Miradi ya Uwajibikaji NMB, Lilian Kisamba, benki hiyo inaamini kuwa ili kupata mafanikio kwa muda mrefu ni lazima itengeneze thamani kwa wanahisa wake na jamii ili kuhakikisha pande zote zinafaidika.

"Tumejitolea asilimia moja ya faida yetu baada ya kukata kodi kufadhili miradi mbalimbali ya kijamii kote nchini. Kadri faida inavyoongezeka, ndivyo bajeti inavyoongezeka.

"Kama kampuni inayowajibika, tumeunda mkakati ambao tunatekeleza kwa sasa ili kusaidia jamii mbalimbali tunakofanyia kazi," alisema.

Kisamba alisema benki hiyo kwa mwaka huu pekee imetenga zaidi ya Sh. bilioni mbili kufadhili miradi ya kijamii kote nchini kwenye maeneo yake ya kipaumbele ambayo imetumika kuchangia vifaa vya elimu, afya na vifaa tiba na vifaa vingine.

"Kulingana na falsafa yetu ya 'Karibu Yako', tutaendelea kujitolea kufanya kazi kwa karibu na jamii tunakofanya shughuli zetu kote nchini ili kuchangia na kuimarisha maendeleo endelevu," Kisamba alisema.

Katika ziara mkoani Njombe hivi karibuni, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Kidegembye, Mary Lihawa alithibitisha kuwa msaada uliotolewa na Benki ya NMB umesaidia kuboresha mazingira ya kusomea shuleni huko.

"Shule yetu ina jumla ya wanafunzi 957, hivyo kwa idadi hiyo kubwa, tulikuwa tukikabiliwa na kero ya uhaba wa madawati kabla ya Benki ya NMB kutunusuru.

"Kwa kweli, wanafunzi takribani saba walikuwa wakitumia dawati moja na hii iliathiri sana mwandiko wao. Kwa msaada wa madawati kutoka NMB, dawati moja kwa sasa linatumiwa na wanafunzi watatu na hii imeboresha sana mazingira ya kujifunzia katika shule yetu," Lihawa aliongeza.

Frank Zambi, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi ya Jangulutu iliyoko Mbarali, alisisitiza kuwa madawati yaliyotolewa na Benki ya NMB kwa shule yake yamesaidia kuboresha ufaulu wa shule kwa ujumla.

Ohadi Nosa, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mgama iliyoko Iringa Vijijini, alisema Benki ya NMB ilisaidia kuweka miundombinu muhimu vya maji na gesi kwenye maktaba ya sayansi ya shule hiyo.

"Mradi wa maktaba ya shule yetu ulikuwa umekwama lakini tulifanikiwa kuishawishi Benki ya NMB kutuokoa na cha kushangaza walifanya hivyo bila wasiwasi wowote." alisema.

Safia Mshana, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Busokelo iliyoko Rungwe, aliipongeza Benki ya NMB kwa msaada wa madawati na meza kwa shule yake na kuongeza kuwa madawati hayo yamesaidia kuboresha mazingira ya kusomea shuleni huko.

Kwa sekta ya afya, Benki ya NMB imetoa msaada wa vifaa mbalimbali vikiwamo shuka, vitanda vya kujifungulia wajawazito na vitanda vya kawaida kwenye vituo vya afya vya Kanda ya Kusini ili kuuunga mkono jitihada za kuboresha sekta ya afya. Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Dk, Darison Sylvand, wilaya yake inahitaji rasilimali nyingi ili kuendeleza vituo vyake vya afya na kuongeza kuwa serikali pekee haiwezi kutoa rasilimali muhimu na kuitaka sekta binafsi kuunga mkono jitihada za wilaya hiyo.

"Tumekuwa tukipokea msaada kutoka kwa benki ya NMB na tunashukuru sana kwa msaada wao. Ninachukua fursa hii kutoa wito kwa wadau wetu kuunga mkono juhudi zetu," alisema.

Zahanati ya Kanyelele iliyoko Rungwe ni miongoni mwa walionufaika na msaada wa vifaa vya afya vya NMB kwa kuwa tayari imepokea vifaa tiba vya kisasa.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kanyelele, Dk. Flumence Kitima alisema vitanda vya kujifungulia vilivyotolewa na Benki ya NMB vilitolewa kwa wakati sahihi kwa kuwa zahanati hiyo inapokea kinamama wengi wajawazito kwa wiki.

"Tunapokea wastani wa kinamama wajawazito sita hadi kwa wiki. Vitanda vya kujifungulia vilivyotolewa na NMB kwa zahanati yetu vimerahisisha kazi zetu kwa kuwa ni vya kisasa na vinavyorekebishwa kiurahisi. Hii inatufanya kuwahudumia wagonjwa kwa urahisi zaidi," alisema.

Maulid Mwingira, Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mbarali alidokeza kuwa benki hiyo imeweka kipaumbele katika sekta ya elimu na afya kutokana na umuhimu wa sekta hizo katika jamii.

Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu wa Benki ya NMB, Straton Chilongola alisema sera ya uwajibikaji ya benki yake inatoa msaada ambapo ujenzi wa majengo utafikia lenta na kutoa vifaa vya kuezekea vyote muhimu ikiwa ni pamoja na mbao, misumari na mabati.

"Hii inatumika kwa ujenzi wa majengo ya shule na vituo vya afya vinavyotafuta usaidizi wetu. Pia tunatoa mahitaji mengine kulingana na ombi maalum," Chilongola alifafanua.

# MAISHA

DESEMBA 18, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14


## KINYWAJI MURUA

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15

Namna ya kupendezesha kitanda






## KATUNIKA

Ukurasa 16




# KATA NYWELE UPENDEZE

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | L | A | A | N | A |
| ■ | A | ■ | ■ | Y | ■ |
| M | W | A | ■ | U | ■ |
| ■ | A | ■ | I | N | A |
| ■ | M | ■ | ■ | G | ■ |
| S | A | U | M | U | ■ |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UGA, SANDA, PENDO, PAGAWA, DANDIA

## AMSHA AKILI

ANGALIA KWA MAKINI KIVULI HIKI, UNAFIKIRI MTU HAYA ANAJIANDAA KWA MCHEZO GANI?



## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kuokota kuni katika pori jirani na nyumba yao. Wakati wanaendelea kukusanya kuni, Juma alimuuliza mama yake.

Juma: Eti mama msemo kila kijani una mti wake una maana gani?

Mama: Mwanangu una maana tofauti, lakini ninayojua ni kwamba kila kitu kina asili yake.

Juma: Kwani hakuna jani bila mti?

Mama: Mwanangu hilo haliwezekani, sawa na mtoto bila wazazi hilo ni jambo gumu

**SWALI**
Zao la korosho linalimwa mikoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mchumba alimrudia mpenzi wa zamani, nimkubali tena?

KARIBU tena msomaji wangu tuserebuke na gurudumu la Maisha Ndivyo Yalivyo. Tupo ukingoni kumaliza mwaka 2022. Je, umejiandaaje kuukaribisha mwaka mpya 2023. Tuombe sana neema ya Mungu ituvushe salama.

Hebu tuendelee kuangaza duru la vijana katika mahusiano. Ndoa nyingi hufungwa miezi inayokaribia kumalizika mwaka. Na ukiona ndoa inafungwa leo, ujue maandalizi yalipitia mchakato mrefu. Kila aliyeoa leo, ana historia ya aliyopitia hadi kuvishana pete ya ndoa!

Wapo wanaotafutiwa wachumba na wazazi wao na wengine hujitafutia wenyewe, kisha kuwashirikisha wazazi. Wengine hupiga magoti na kumshirikisha Mungu kuwachagulia wenza wa kuishi nao.

Kundi hili hufanikiwa sana kwani wanajua siri ya kuchagua kama nilivyoeleza wiki moja iliyopita, "nguvu ya kuchagua ilivyowaweka wengi mtegoni.

Kila mtu anayo nguvu ya kuchagua ambayo Mungu ameweka ndani yake. Akasema kwenye neno lake, "Nazishuhudia mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimeweka mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima ili uwe hai, wewe na uzao wako".

Msomaji wangu, kumbuka kuchagua ni kupanga. Vijana wengi wamekuwa wanadhani kuoa ni lelemama, ni fasheni. Hapana. Ni mtihani uliojaa mafumbo mengi. Kijana mmoja akaniambia, "mama, napitia mambo magumu katika mahusiano. Natamani mwakani nioe lakini sioni upenyo. Nilikuwa na mpenzi wangu nampenda sana. Nilipanga kuoana naye mwakani, lakini baadaye akabadilika. Akaniambia yupo mpenzi wake wa awali amemuomba msamaha warudiane. Aliposema hivyo nikamwambia ni sawa!

Baada ya hapo mimi nikakata mahusiano naye. Cha ajabu siku hazikupita nyingi, akamtuma rafiki yake kwangu kwamba anahitaji niende kwake. Je, nifanyeje wakati alinisaliti? Na tangu tuachane sijahangaika naye tena, hata akinikuta njiani hanisabahi, nami namuacha kwani yeye ndiye aliyeleta vituko.

Bila shaka msomaji umempata vema kijana huyu kuhusu mapito yake katika mahusiano. Aliweka tumaini kwa msichana lakini akambadilikia.

Nafsi ya mtu imeficha mengi. Lile unalomuwazia mwenzio, siyo analokuwazia wewe. Yupo anayekuwazia kukuua kiuchumi lakini wewe hujui, ila Mungu anajua.

Ndiyo maana nasisitiza kwamba mshirikishe Mungu jambo lako usiamue peke yako atakuepusha na mengi. Atakuchagulia yule anaona ni sahihi kwa maisha yako!

Kijana alidhani kapata kumbe ni mke wa mtu mwingine. Aliyempata akamwambia amemrudia mpenzi wa awali. Ukiona mambo ya aina hii, ujue lipo jambo kaepushwa. Pengine hata kama angemuoa, bibie bado angeendeleza mahusiano na huyo wa zamani. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Kiukweli hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya. Kila jambo lina kusudi au chanzo. Yawekana kabisa kijana anaepushwa kitu.

Jiulize, kama alimuacha mpenzi wa zamani, atashindwaje kumuacha huyu katika ngazi ya uchumba au baada ya kumuoa? Hapa mtu ni lazima ajiongeze. Au siyo msomaji?

Binti huyu inaonekana anashambuliwa na roho ya kuacha na kuachwa ndani ya familia au ukoo wake. Hata ikitokea kijana huyu kumuoa, bado roho ya kuacha itaendelea na mwishowe atabaki anajilaumu. Kumbe alipaswa kuamua mapema kujinasua.

Ipo tahadhari ambayo Mungu ameitoa katika moja ya maandiko yake kwamba, "Unaona mambo mengi, lakini huyatilii moyoni, masikio yake ya wazi, lakini hasikii".(Isaya 42:20).

Mungu ameweka wazi. Na kwa kijana dalili za kuja naye kuachwa ziko wazi kwa sababu binti huyu ni kigeugeu. Hana maamuzi kwani ipo roho inayomtawala.

Roho ya kuacha na kuachwa inafanya kazi katika mahusiano ya vijana hawa pasipo wao kujua au kujitambua. Ndio maana binti anatoka pale anarudi huku, anarudi huku, kisha anarudia pale.

Roho hii inaambatana na roho zingine mbili hivi. Roho ya kutanga-tanga na roho ya mitala (kuoa wake wengi au kuolewa na wanaume zaidi ya mmoja). Hili ni tatizo kubwa ambalo linaweza kuharibu utaratibu au mfumo mzima wa maisha yake.

Msomaji wangu, tatizo la vijana kuachana kabla ya kuoana ni dalili kwamba hata wakilazimisha baadaye kuoana, uwezekanao wa kuachana siku za usoni ni mkubwa kwa sababu ya hiyo roho.

Mifano ni mingi sana kwa wale wanaokutana na majaribu wakati wa uchumba na wakioana ndoa zinavunjika. Kumbe chanzo kimeanza kwa wazazi wao au ukoo.

***Chunguza jiridhishe kabla ya kujitoa kuoa au kuolewa kuepuka majuto! Je, una kisa? Ujumbe 0715268581***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tutunze mazingira kwa nguvu zote kuepuka kuangamia

MOJA ya matatizo makubwa yanayoikabili dunia na Tanzania, ni kasi ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha kukosekana kwa mvua za kutosha, ukame, mafuriko na madhara mengine yanayotishia uhai wa watu.

Mabadiliko ya tabianchi hayasababishwi na eneo fulani pekee bali mchango wa dunia kwa ujumla huku nchi za Afrika kwa ujumla wake, zikichangia hewa ya ukaa chini ya asilimia nne na nchi zilizoendelea zikichangia kwa kiasi kikubwa.

Kwa sasa, hali ya upatikanaji wa maji ni ngumu hususan Dar es Salaam na imefikia yanauzwa Sh.1,000 kwa galoni la lita 20 hali inayoongeza ugumu wa maisha. Hali hii ni kutokana na kutegemea mvua kama chanzo cha kupata maji kwa sababu yanachukuliwa kwenye mito na kuna visima vichache.

Mathalani, kwa Tanzania, mtu mmoja anachangia gesi ya ukaa kwa asilimia 0.22 kwa mwaka, huku China na Marekani akichangia asilimia 26 kwa kipindi hicho hicho kutokana na shughuli za viwanda na nyinginezo ndiyo maana nchi hizo zinatoa fedha za kusaidia kukabili kwa nchi zilizotunza mazingira.

Hadi sasa hakuna mpango kwa nchi hizo kupunguza viwanda,ndio kwanza vinaongezeka na zipo tayari kuendelea kutoa fedha kwa nchi zinazochangia kupunguza hewa ukaa kwa kutunza mazingira.

Kwa sasa, kila eneo linakabiliwa na ukame huku maji ambayo ni muhimu kwa kila kiumbe, yakiendelea kupungua. Migogoro baina ya binadamu na binadamu; wanyama na binadamu, inaongezeka kwa sababu rasilimali hiyo inapotea katika baadhi ya maeneo.

Ukisafiri kwa anga, utaona hali ilivyo ardhini lakini kasi ya kupaa kwa bei ya nafaka kulikochagizwa na kupaa kwa bei ya mafuta ni udhihirisho kwamba ukame ni tishio. Pia unaona mito na maeneo mengine yalivyokauka.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilieleza mwelekeo wa mvua kuwa si wa kuridhisha. Wakulima wameshauriwa aina za mazao ya kulima ambayo ni ya muda mfupi na yenye kuhimili ukame.

Hadi sasa tunaona uhaba wa nafaka huku ikizidi kupanda bei, ongezeko la migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ambao wanatoka maeneo yaliyohifadhiwa kwenda kutafuta malisho, huku binadamu nao wakivamia maeneo ya hifadhi kupata mahitaji ya wanyama wafugwao.

Jitihada nyingi zimefanyika ikiwamo kuhamasisha wananchi kutunza mazingira, kupanda miti kwa wingi na kuachana na matumizi ya nishati ya kuni, ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa kuwa mkaa unatumika zaidi kutokana na kupaa kwa bei ya gesi.

Hali ya upatikanaji wa chakula ni ngumu sana kwa sasa,nafaka zimepanda bei hali ya maisha inakuwa ngumu kutokana na visababishi vingine kama kupanda kwa bei ya mafuta na COVID-19.

Mabadiliko ya tabia nchi si jambo la kulichukulia rahisi,lazima nchi iendeleze mikakati yake ya kusaidia wananchi wake kuishi na hali hiyo ambayo haiwezi kuisha leo wala kesho kutokana na kasi ya ukuaji wa maendeleo.

Lazima jamii yetu iendelee kuelimishwa namna ya kutumia fursa katikati ya matatizo, mathalani kwa sasa kuna biashara ya hewa ukaa kwa wananchi waliotunza misitu ya asili,misitu ya kupanda na binafsi ambayo wanauza duniani kwa nchi zilizoharibu au zinazoharibu mazingira.

Misitu hiyo inasaidia kupunguza hewa ukaa kwenye anga na kukabili hali iliyopo sasa ya vipindi vya mvua kutoeleweka,ukame wa muda mrefu,joto na bariki kali kiasi cha kuathiri binadamu na viumbe wengine kama tunavyoona sasa maeneo mengi yana joto kali hadi misitu inawaka yenyewe na kwingine baridi sana.

Kwa sasa usalama wa chakula uko hatarini kwa kiasi kikubwa,kwamba wananchi hawana uhakika wa mlo kamili kutokana na kwamba hawana uhakika wa chakula chenyewe ili waendelee kuwa hai.

Kwa mantiki hiyo, kupambana na mabadiliko ya tabia nchi ni lazima kwa kila mmoja lakini wananchi kutumia mbinu zao na za jumla kukabili hali hii,ili dunia iwe salama kwa kila mmoja anayestahili kuifurahia.

Kwa sasa tunasikia migogoro baina ya wanyama na binadamu inashamiri,wanyama wanatoka kwenye maeneo yao ya asili kutafuta malisho na binadamu anapeleka mifugo maeneo yaliyohifadhiwa kutafuta malisho,hii inafanya maisha yasiwe na amani kwenye maeneo mengi.

Mabadiliko ya tabianchi ni tishio lazima tuwe na mbinu zinazotekelezeka, kubuni namna ya kuendelea kupata maji ya mahitaji ya nyumbani na kilimo cha umwagiliaji kwa sababu cha mvua hakijaonyesha manufaa chanya.

# HARUSI







FAMILIA ya Patson Mlandali na mke wake Caren Mgonja ilikuwa siku ya furaha kwao baada ya binti yao Diana kupata sakramenti ya kipaimara katika kanisa la KKKT Yombo Kilakala. Sherehe fupi ilifanyika nyumbani kwao Yombo mkoani Dar Es Salaam hivi karibuni.







## MITINDO

# WANAUME WALITISHA 2022







2022 umekuwa na maendeleo makubwa katika suala la ubunifu wa mavazi.

Mavazi kama nguo za kitamaduni, suruali za vitambaa, jinz na nguo za michezo yalitawala sehemu mbalimbali.

Hata hivyo aina hiyo ya mavazi itaendelea kuimarishwa zaidi mwaka unaokuja na kutarajiwa kuwa na aina mpya ya mitindo ambayo itafurahisha wengi.

Hakuna aliyepata shida kwa kukosa aina ya nguo anazopenda ndani ya mwaka 2022, hivyo kila mahali ilitawala furaha.

Katika majira ya joto, kaptura zilishika nafasi na kufanya kampuni nyingi kubuni na kutambulisha aina mpya ya nguo hizo.

Mchanganyiko wa kaptura na suruali za kawaida nazo zilitamba na kuwafanya watu kuwa na machaguo mengi ya namna ya kuvaa nguo.

Mchanganyiko wa rangi na mitindo ya kibunifu imewafanya watumiaji kuchizika kwa kila wakati kununua nguo za kuvutia na za kipekee.





UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# KATA NYWELE UPENDEZE

KUKATA nywele ni moja ya aina ya urembo ambao unabadili mwonekano wa mtu na kumtambulisha umaridadi wake.

Kama ilivyo kwa nywele ndefu, hata fupi nazo zinahitaji matunzo na kutengenezwa kila siku ili kuzifanya zionekane vizuri.

Mwanamke mwenye nywele fupi anatakiwa kuongeza nakshi za kuongeza rangi, kupaka dawa ya kulainisha na mafuta kuzing'arisha.

**Mambo ya kuzingatia**

Kwa mwanamke mwenye nywele fupi anatakiwa kuzipunguza mara kwa mara angalau kila baada ya wiki mbili ili kubaki na mwonekano wake.

Hata hivyo, kama unataka kubadili aina na ukubwa wa nywele zako unaweza kufanya hivyo.

Ukiwa na nywele fupi pia unatakiwa kuzingatia aina ya hereni unazovaa, ziwe zinakupa muonekano mzuri kwa kuzingatia pia aina ya vazi ulilovaa.

Zingatia pia kupaka rangi ya midomo kama nyekundu, pinki na nyingine ambazo zinakupa mwonekano wa kung'aa usoni.

Unaweza pia kunogesha nywele zako kwa kupaka black au breach na kuweka mstari pembeni ili kubadili mwonekano wako.





MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

KINYWAJI MURUA

# Juisi ya tangawizi, pasheni

TANGAWIZI ni kati ya viungo mahiri vinavyochochea ladha nzuri katika vyakula vya aina mbalimbali na hivyo kuwavutia walaji kula chakula husika.

Tangawizi pia inapowekwa kwenye vyakula vigumu kama nyama huifanya ilainike na hivyo kuweza kuiva kwa haraka zaidi.

Leo katika safu ya mapishi nitaeleza jinsi ya kutengeneza juisi ya Tangawizi.

**Mahitaji**

Unahitaji tangawizi vipande 10, maji lita moja, sukari au asali kiasi na pasheni ili kuongeza ladha ya juisi yako.

**Namna ya kuandaa**

Safisha vizuri tangawizi zako bila kuzimenya na weka kwenye brenda uchanganye na maji.

Anza kusaga mpaka zilainike na baada ya hapo chuja na weka pembeni.

Chukua pasheni tatu, anza kuzisaga kidogo hakikisha mbegu hazilainiki.

Baada ya kusaga changanya na juisi yako ya tangawizi, tayari kwa kunywa na familia yako.

Ukiona tangawizi imekuwa kali sana unaweza kuongeza kiasi kidogo cha maji upate ladha unayotaka.

**Faida zake**

Tangawizi hutumika kama kituliza maumivu na husaidia kuboresha mmeng'enyo wa chakula tumboni.

Kadhalika huthibiti shinikizo la damu, huboresha afya ya kinywa, hukinga matatizo ya ngozi hasa chunusi na husaidia kuimarisha afya ya nywele.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Tumia ubunifu kurembesha chumba cha kuvalia

SEHEMU ya chumba kinachotumika kuvalia nguo (dressing room) ambacho pia wengi hutumia pia kupumzika, ni muhimu na ndiyo mahali pekee ambapo huchangia kumtoa mtu akiwa amependeza au amechukiza.

Watu wengi wanaokuwa wamependeza wanapotoka ndani na kuvutia machoni pa watu husifiwa kwamba wamependeza, siri yake huwa ni chumba maalum ambacho hutumika kuvalia.

Kutokana na umuhimu wake, kuna haja kubwa ya kuhakikisha kinawekwa katika mazingira mazuri ya kuvutia kama ambavyo watu wanaokitumia hutoka humo wakiwa wamependeza na kusifiwa na watu na kujiona 'babu kubwa'.

Nafahamu kwamba kabla ya kupangilia chochote katika chumba hiki, kitu cha kwanza kabisa ni kitanda kikifuatiwa na vitu vingine.

Leo nimeona nizungumzie namna ya kupangilia chumba hiki katika mtindo wa kama sehemu pia inayotumika kwa ajili ya kuvalia.

Mbali na kitanda kuwekwa na mpangilio wake maalum , lakini lazima tuhakikishe kwamba vitu vingine vinavyokipamba navyo vinawekwa katika utaratibu mzuri unaoeleweka na si tu kuweka kama pango la wanyang`anyi.

Vitu vya muhimu vya kuzingatiwa vya kusaidia kupamba chumba hiki na kithaminike kuwa kinasaidia kumtoa mtu akiwa amependeza ni pamoja na kuhakikisha kupangilia vifaa vyote katika eneo lake vinavyowekwa kwenye chumba chako hicho.

Miongoni mwa vinavyotakiwa kupangiliwa vizuri katika chumba hiki ni kabati la nguo kwa sababu ndilo hutumika katika kuhifadhia nguo na pia unapokuwa nalo linasaidia kupunguza mlundikano hovyo wa nguo ambao unaweza kuwapo.



Hakikisha kabati lako linawekwa sehemu ambayo ni sahihi, kama ni la ukutani au la kusimamisha kawaida, hakikisha linawekwa sehemu sahihi ambalo pia haliwezi kufinya nafasi ya kuwekwa kitu kingine.

Katika mpangilio wa kabati unapaswa kuangalia sehemu sahihi ya kuliweka, aidha liwe la ukutani au la kusimama kawaida.

Kitu cha pili ni kuangalia namna ya kupangilia 'dressing table' yako. Hapo pia unapaswa kuwa mbunifu kwa kuangalia eneo sahihi ambalo pia itakuwa rahisi kwa matumizi yako.

Kingine ni mpangilio wa pochi, hizi nazo zinapaswa kutundikwa katika stendi yake maalum katika eneo lake maalumu.

Mbali na hivyo, kingine ni mpangilio wa viatu, hivi navyo vinatakiwa viwekwe katika mpangilio mzuri ili visiharibu muonekano wa chumba.

Ikiwezekana, hakikisha unaandaa fremu maalum kwa ajili ya viatu tu na ikiwezekana vipangiliwe kulingana na muundo wake ili kuongeza mvuto, kama ni virefu viwekwe kwa mpangilio wake na vifupi hivyo hivyo.

Jambo ninalotaka kusisitiza hapa ni kwamba si vibaya kama kila kitu kinachowekwa katika chumba hiki kinazingatia rangi za vitu vilivyopo katika chumba hicho, kwa sababu hii ni nyezo muhimu katika kunogesha chumba.

## Namna ya kupendezesha kitanda



MWONEKANO wa kitanda kilichokamilika kwa ajili ya kulala ni kuwa nadhifu kutokana na muunganiko wa matandiko mengi.

Je vitu gani vinafanya kitanda kuwa nadhifu na kionekane na mvuto? Hizi ni baadhi ya dondoo zitakazokusaidia kupendezesha kitanda.

### MITO

Mito safi hufanya kitanda kionekane maridadi, epuka mafuta na uchafu kutoka kwenye nywele na nyuso zetu zinazama hadi kwenye sponchi ndani na kuharibu mto. Kuzuia uchafu huu usizame kwenye mto basi unatakiwa uwe unaufua japo mara moja kila mwezi au kila baada ya miezi miwili.

### SHUKA

Kipindi unachotakiwa kufua shuka baada ya kuzilalia mara nyingi hutegemeana na uamuzi binafsi. Lakini ni vyema shuka ukazifua kila unapoona zimechafuka ili kitanda kiwe safi.

### BLANKETI

Kutandika blankenti ni aina nyingine ya kupendezesha kitanda, lakini tandiko hilo lazima liwe safi.


Kama una blanketi la kupambia kitanda tu na wala halikunjuliwi na kutumika, basi kulifua kila baada ya miezi kadhaa itakuwa sahihi. Ila kama linatumika kila unapolala unaweza kulifua kila baada ya majuma matatu.

### KOMFOTA

Wengi wanatumia komfota na duveti kama tandiko la juu la kupendezesha kitanda.

Kama unatumia tandiko hili kila wakati na kama halijamwagikiwa chochote unatakiwa kulifua zaidi ya mara moja au mbili kwa mwaka.

# KATUNI


JUKWAANI
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
HALOOOOOOOO!!!
AJALI
BABY YAANI MUME WANGU KARUDI SAFARI "KAUONA MZIGO" KACHEKELEAJE? KATHEMA KITANDA HAKIDHAI HARAMU
KWA HIYO MMENIFANYA NG'OMBE?
NDANI YA KIBASI
ACHENI KEBEHI, KWA WALIO-JENGA BONDENI KWANI WAO WAMEOMBA?
WAKATI WANAUZIWA HAWAKUJUA KAMA WANANUNUA HATARI? AU TAMAA ZA KUWA KATIKATI YA MJI?
WEWE USTAKE KULETA KUFURU
HIYO MADA YENU NTAWASUSIA GARI MUENDESHE!..OHOO!
KUFURU IPI?
BASI SUKA HATUJAJUA KAMA NAWE MUHANGA WA MABONDENI.
KWANI KUJENGA NI KAMA DHARURA INAKUJA GHAFLA?
MANENO MATAMU YA DALALI NAYO!
TAZAMENI MTAPIGIKA KUKEJELI MAISHA YA WATU.
KITAA CHA KWET
HATA DAGAA NAO NI SAMAKI USIJIFOSI DADA.
NINI DAGAA... HATA NGADU NAE SAMAKI MBONA HUNA?
WEKA HAPO HELA YA KADI ELFU TANO. KUMUONA DOKTA ELFU ISHIRINI... KAMA HUNA TOKA! WAPISHE WENZAKO
NIPO KWA MGANGA, AU NIMEKUJA HOSPITALI KUMUONA DAKTARI BINGWA?
WAHUDUMU WAKO WABAYA SANA! ETI NIMEINYWEA NAULI HAWANIGUTUSHI.
HATA UNGE-NYWEA HELA YA SANDA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MZIGO WA MAWAZO HAUBEBWI NA KULI...



Wafanyakazi wa uokoaji wakipambana kuzima moto katika jengo la makazi katika mji wa Kyiev baada ya kushambuliwa na makombora ya Russia jana. **PICHA: REUTERS**

# Ukraine sasa yawa motoni usiku, mchana yashambuliwa

**KYIEV,** UKRAINE

RUSSIA inazidi kuiteketeza Ukraine kwa makombora yanayorushwa usiku na mchana na kusababisha miji yote mikubwa kuwa katika hali mbaya.

Msemaji wa jeshi la angani la Ukraine Yurii Inhat, alisema zaidi ya makombora 60 yalirushwa na kuilenga miji kadhaa nchini humo.

Katika taarifa zilizotolewa na maofisa wa serikali Russia imefanya mashambulizi katika miji mitatu Kiev na kuteketeza vituo vya nishati na miundombinu mingine.

Iliripotiwa kwamba tayari mashambulizi hayo makubwa yameathiri mfumo wa usambazaji maji katika mji huo mkuu.

Watu wawili wameripotiwa kuuawa kufuatia shambulizi la roketi dhidi ya makazi ya watu katika mji wa kusini Kryvyi Rig na wengine watano wamejeruhiwa wakiwemo watoto wawili.

Kiongozi wa mji huo Valentyn Reznichenko, alisema maeneo kadhaa yalikosa umeme kutika mashambuzli hayo.

Meya wa Kharkiv, Ihor Terekhov alisema kupitia ukurasa wake wa Telegram kwamba mji wake hauna umeme wala maji.

Gavana wa jimbo la Kharkiv, Oleh Syniehuboy, alisema mashambulizi matatu yalifanywa dhidi ya miundombinu mitatu ambayo ni muhimu kwa mji huo.

Kyrylo Tymoshenko, ofisa wa ngazi ya juu katika ikulu ya Rais Volodymyr Zelensky, aliripoti kwamba shambulizi moja lililenga jengo la raia katika mji wa Kryvyi Rih.

Kupitia ukurasa wake wa Telegram, alitahadharisha kwamba huenda kuna watu wamefunikwa kwenye vifusi vya jengo hilo lililoporomoka baada ya kushambuliwa. Waokoaji wanaendelea kufukua vifusi hivyo.

Hata hivyo, raia wameshauriwa kutafuta maeneo salama zaidi kunusuru maisha yao.

"Mashambulizi dhidi ya mji mkuu yanaendelea. Huduma za usafiri wa reli zimesitishwa, Alisema.

Alisema hayo huku baadhi ya raia wa mji huo wakikimbilia njia za chini ya ardhi za treni kujificha dhidi ya mashambulizi.

Kwa mara ya kwanza mji mkuu Kiev ulielekezewa makombora mengi zaidi kuwahi kushuhudiwa tangu mwanzo wa uvamizi huo Februari 24.

Takriban makombora 40 yamerekodiwa katika anga ya mji huo.Hayo ni kulingana na taarifa ya maofisa wa mji huo. Kampuni ya taifa inayosimamia reli nchini Ukraine Ukrzaliznytsia ilisema umeme umekatika katika vituo vingi vya treni mashariki na maeneo ya kati mjini Kharkiv, Kirovohrad, Donetsk na Dnipropetrovsk kufuatia mashambulizi dhidi ya miundombinu ya kuzalisha nishati. Hata hivyo katika maeneo mengine, treni zimeendelea kuhudumu kwa kubadili mifumo yao, kuachana na injini ya umeme na kutumia injini au mitambo inayoendeshwa na mvuke.

Mji wa pili kwa ukubwa Ukraine Kharkiv jana ulisalia bila ya nishati ya umeme baada ya wimbi la mashambulizi ya Russia.

Maofisa katika mji huo walisema takriban vituo tisa vya nishati vilishambuliwa wakati vikosi vya Russia vilipofyatua makombora 76 na ndege zisizo na rubani.

Meya wa Kharkiv alisema mji huo umeharibiwa kwa kiasi kikubwa.

Kufikia jioni, asilimia 55 ya wakazi wake walipata huduma ya umeme.

Mkazi mmoja, aliliambia BBC kwamba mashambulio hayo yalianza kwa ukali.

"Dakika chache, taa zilianza kufifia,sekunde kumi tu baadaye, umeme ulipotea, kila kitu kilitulia, alisema mkazi huyo.

Aliongeza "Kwa sasa hakuna maji pia kwa sababu vituo vya kusukuma maji haviwezi kufanya kazi wakati hakuna umeme mjini, kwa hivyo tulichonacho sasa ni mji usio na maji wala umeme."

PUTIN MKUTANONI

Ikulu ya Russia ya Kremlin, ilitangaza kwamba Rais Vladmir Putin amefanya mkutano na makamanda wa majeshi kujadili mapendekezo ya mbinu ya kuendeleza mashambilizi yake nchini Ukraine.

Putin aliongoza kikao kilichohudhuriwa pia na Waziri wa Ulinzi, Sergei Shoigu pamoja na mkuu wa majeshi Valery Gerasimov.

Ufaransa na Umoja wa Ulaya zimesema kwamba mateso wanayopata raia wa Ukraine ni uhalifu wa kivita, huku mkuu wa sera za kigeni wa umoja huo Josep Borrell akiyataja mashambulizi hayo ya mabomu kuwa sawa na unyama

***DW***

## Watu 160 walikufa mafuriko DRC

**KINSHASA**, DRC

MAOFISA wa Umoja wa Mataifa wanakadiria kwamba zaidi ya watu 160 wamekufa katika mafuriko mabaya yaliyoukumba mji mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wa Kinshasa.

Ofisi ya Umoja huo ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) ilisema kufikia Desemba 16, mamlaka za DRC ziliripoti kwamba angalau watu 169 walikufa na wengine karibu 30 walijeruhiwa.

Ilielezwa nyumba 280 ziliharibiwa na mafuriko hayo. Serikali haijatangaza ongezeko la idadi ya watu waliofariki tangu ofisi ya waziri mkuu ilipotaja idadi hiyo kuwa watu 120 Jumanne.

## Trump azidi kubanwa vurugu 2021

**WASHINGTON,** MAREKANI

UCHUNGUZI wa bunge kuhusu ghasia za mwaka jana katika bunge la Capitol, utaripoti kupendekeza mashtaka matatu ya uhalifu dhidi ya rais wa zamani Donald Trump.

Kamati teule ya Baraza la Wawakilishi itatafuta mashtaka ambayo hayajawahi kushuhudiwa ya uasi dhidi ya rais huyo wa zamani wa Marekani, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Marekani.

Jopo hilo linatarajiwa kuchapisha ripoti yake ya mwisho wiki ijayo.

Wafuasi wa Trump walivamia Congress mnamo Januari 6, 2021 kwa nia ya kusimamisha uidhinishaji wa jina la Joe Biden kama rais.

Idara ya haki ambayo tayari inachunguza jukumu la Trump katika machafuko hayo,hailazimiki kuzingatia rufaa kutoka kwa jopo lolote la bunge.

Kamati teule imeratibiwa kufanya mkutano wake wa mwisho kesho wakati mapendekezo yoyote ya kesi yatabainika.

Kulingana na vyombo mbalimbali, jopo hilo litapendekeza Trump ashtakiwe kwa kuzuia utaratibu rasmi na kula njama ya kulaghai Wamarekani.

## MAKALA

# ITAFUTWE DAWA YA KUDUMU KATIKA HILI



Na Magabilo Masambu

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa anafanya ziara maeneo mbalimbali ya nchi katika kukagua miradi ya maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma zilizokusudiwa na serikali.

Katika ziara hizo, Majaliwa amekuwa akiibua madudu juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye baadhi ya halmashauri. Tumeona baadhi ya maeneo watumishi wa umma wanatuhumiwa kuchoma ofisi za umma ili kupoteza ushahidi wa nyaraka muhimu kuhusu utekelezaji wa miradi ambayo haijakamilika. Pia katika maeneo mengine, tumeshuhudia baadhi ya watendaji wa serikali wakijimilikisha mali za umma kinyume cha sheria na taratibu za nchi.

Swali linasalia je, kwa jinsi hali ilivyo vita hivi Waziri Mkuu pekee yake ataweza? Je, njia ya kumkaba mtumishi mmoja mmoja itakuwa njia ya kudumu ya kumaliza tatizo nchini? Ni dhahiri kwamba inaweza kuwa isiwe rahisi kumaliza tatizo bali kuwafanya watumishi wa aina hiyo kutafuta njia mapema za kuzunguka wakiwa wamefanya matumizi mabaya ya mali za umma.

Jambo hili linagusa masilahi ya umma moja kwa moja na lazima kama taifa kufikiria njia thabiti na ya kudumu kushughulika na jambo hili. Waziri Mkuu ni mmoja ambaye naamini hataweza kufika kila mahali na kila ofisi ya umma kukagua ubadhirifu na uharibifu wa mali za umma. Kila mahali anakokwenda, inaonekana kuna matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Kuna baadhi ya miradi imemaliza zaidi ya mwaka wakati fedha zilitolewa, kuna mahala mfano waliambiwa kujenga majengo kadhaa, fedha zilitolewa za majengo hayo lakini mejengo yako pungufu na fedha zimekwisha. Je, ni kwamba fedha zinazotolewa na serikali kwa baadhi ya miradi huwa hazitoshi kukamilisha miradi hiyo?

Kuna wakati nilizungumza na mkuu mmoja wa shule akanieleza kwamba kuna wakati wanalazimika kutumia pesa zao za mfukoni kukamilisha miradi. Sababu anayotoa ni kwamba fedha kwa baadhi ya miradi zinaletwa kidogo tofauti na gharama halisi za ujenzi lakini mradi usipokamilika unaulizwa kwa nini fedha zilikuja na hukukamilisha mradi? Kama lipo hilo ni muhimu serikali kulitazama ili wakati mwingine watendaji wasije kuwa wanatuhumiwa kwa wizi mbele ya wananchi kumbe wanaogopa kusema kwamba pesa zilizoletwa hazitoshi.

Pamoja na yote hayo, lazima tuwe na mfumo utakaojiendesha wa kuzuia wizi wa mali za umma. Kuna wakati kwenye serikali za mitaa tulikuwa na viongozi mchanganyiko kutoka vyama vingine vya siasa, lakini ikaonekana kwamba wanakwamisha maendeleo na kwamba tukiwaondoa tutafanya maendeleo kwa kasi. Inawezekana mtazamo huu haukuwa sahihi kwa sababu wizi na ubadhirifu huu unafanyika tukiwa wenyewe na inaweza ni sababu mojawapo maana tukizungumza tunaelewana hakuna wa kusema hapana jamani hizi ni fedha za wananchi!

Jambo la kwanza, ni lazima tujiulize kwa nini watu wanafuja fedha bila kuogopa? Ni hivi karibuni tu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilitaja watu wengi tu kwa ubadhilifu wa fedha za umma lakini ni kwa kiwango gani hatua zimechukuliwa?

Kama hazikuchukuliwa tatizo liko wapi? Hili la mtumishi kuharibu hapa na kuhamishiwa sehemu nyingine limefanikiwa kwa kiasi gani kupunguza wizi na madudu? Mfano yule ofisa mipango miji aliyemtaja Waziri Mkuu kwamba alikuwa mahali akafanya madudu akahamishiwa halimashauri nyingine, akaenda kufanya yale yale na zaidi hili limekaaje?

Mifumo yetu ya kisheria imekaaje katika kushughulikia masuala kama hayo? Nani anafuja na nani anachunguza? Wananchi wamepewa nafasi gani ya kusimamia fedha zinazotokana na kodi zao kupitia Bunge? Je, wabunge wanafanya kazi ya kibunge sawasawa katika kusimamia masuala yanayowahusu wananchi? Suala la uwajibikaji itokeapo tuhuma kama hizo linakuwaje? Ni nani yuko tayari kuwajibika kwa hiari yake?

Mpaka yanatokea haya, madiwani kwenye halmashauri zetu huko wana nguvu kiasi gani kusimamia maslahi ya wananchi kupitia vikao? Pamoja na majukumu mengine, pamoja na kusimamia vyema fedha za miradi na kuhakikisha miradi inakamilika kwa maelekezo ya serikali au kushauri kama fedha zinazokuja hazitoshi kukamilisha? Wengi pengine wana nia ya dhati ya kusimamia lakini pengine wanaogopa kufanya hivyo kwa sababu wanategemea kupitishwa na watu fulani kwenye kura za maoni ndani ya chama ili waombe ridhaa ya kuchaguliwa tena kwa hiyo wanaogopa na badala yake wanakuwa ndiyo mzee?

Wakati mwingine namwonea huruma Waziri Mkuu maana mfumo ukishakuwa hivyo, mwisho wa siku itakuja kuonekana kama ni jambo lake binafsi wakati anatekeleza kazi yake kama mtendaji mkuu wa serikali, waharifu wakishakuwa wengi kwenye mfumo watu wenye nia njema na nchi hugeuka kuwa maadui na kuundiwa zengwe unatembea na watu kwenye ziara na kudhani mko pamoja wao ndiyo wanakuwa wa kwanza kupiga simu kwamba anakuja fanyeni hivi na vile.

Ni muhimu kama nchi kujitafakari na kutafuta njia ya kudumu itakayowafanya kama siyo watu wote ndani ya nchi basi asilimia kubwa kuwa na uwezo wa kuchukia ubadhirifu na kupigana vita kwa pamoja maendeleo ya nchi si ya mtu mmoja ni ya wote kwahiyo ili tuweze kufanikiwa kila mtu kwa uwezo wake anapaswa kushiriki tusiseme hili si letu ni lenu?

**0689157767**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Msondo wanaonya, kumpenda mke wa rafiki yako ni hatari*



Na Adam Fungamwango

WAKATI kuna baadhi ya nyimbo kisasa zikijinasibu na kujigamba kuwa nyumba ndogo na wala hazioni tatizo kumchukua mume au mpenzi wa rafiki au shoga wa mwenzake, wanamuziki wa zamani walipinga sana hilo.

Walihubiri amani. Ukitaka kuishi kwa amani fuata miongozo yote na sheria ambazo zinatolewa na dini pamoja na serikali. Ili nchi, jamii, au himaya iishi kwa amani, ni lazima kila mmoja afuate miiko, kanuni na miongozo yote iliyotolewa na anayekiuka, basi adhabu inachukua mkondo wake.

Kila nchi, eneo, jamii au himaya ina adhabu zake kwa jinsi wenyewe walivyojiwekea.

Ndani ya jamii kuna mambo mengi sana. Kila mmoja ana mpenzi wake na kila mmoja ana mume au mke. Lakini kuna baadhi ya watu wamekuwa na tamaa. Ana mke au mume, lakini bado ana tamaa kwa wa mwenzake. Wengine hawana waume wala wake, badala ya kusaka wao, wao wanachukua wa mwenzao.

Hii imeleta migogoro, uhusiano mbaya, ugomvi, hata maafa kwa baadhi wanaobainika kufanya hivyo. Dunia hii ni pana, na hakuna mtu wa kuimaliza. Kila mmoja anaweza kuwa na mpenzi, mume au mke na hakutokuwa na shida yoyote ya kuingiliana au mtu kumchukua wa mwenzake.

Kinachosababisha hivyo ni tamaa ya binadamu. Ndiyo maana hata mababu wa zamani akimkalisha chini mjukuu wake atamwambia afanye vitu vyote, lakini si kuchukua mke wa mtu.

Acha hao kuna wengine wanakwenda kuchukua mpenzi, mke au mume wa mtu ambaye anamfahamu kabisa. Wakati mwingine ni rafiki yake kipenzi. Hii si tabia mbaya tu, bali ni ya hatari. Mambo haya yanatokea sana kwenye jamii. Na ndiyo maana tunaona hata sasa kwenye vyombo vya habari, magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wanachukua uamuzi mgumu.

Ni uamuzi ambao si wa kuuendeleza wala kuufuata kwa sababu ya hatari, lakini chanzo chake ni watu wenye tamaa. Tabia hii haikuanza leo. Ni tangu enzi na enzi. Ndiyo maana wanamuziki wa dansi wametunga nyimbo mbalimbali za kuionya jamii kuhusu tabia hiyo.

Leo tutaziangalia nyimbo mbili zote zikipigwa na Msondo Ngoma. Moja ilipigwa wakati ikiitwa Juwata Jazz Band na nyingine wakati imeshabadilishwa jina, ikiitwa OTTU Jazz Band. Tuanze na wimbo wa 'Ushinde Moyo Wako'. Ulipigwa katikati ya miaka ya mwanzoni mwa miaka ya 1990, wakati ikiitwa OTTU Jazz.

Inasimulia kisa cha kijana aliyekuwa akitembea na mke wa rafiki yake. Mmoja wa rafiki zake alipogundua hilo akamfuata na kumkanya kuhusu kitendo chake hicho kisicho cha kiungwana. Akamwambia maneno haya ambayo yamo kwenye wimbo huu.

"Usiendekeze moyo utakavyokutuma, unadanganya jaribu kushinda, usiposhinda huna budi kuumia, utajivika kitanzi pasipo huruma.

Kumpenda mke wa rafiki yako mpenzi ni hatari, viko vitu vya kupenda lakini vingine vina madhara, ooh moyo utakupeleka kaburini.

"Nakuomba jirekebishe bwana, tabia hiyo siyo nzuri bwana, ni kitendo cha aibu na kashfa ya hali ya juu, ninakusihi bwana acha mara moja.

Ulijua ya kwamba ni shemeji yako baba, wa rafiki yako swahiba na leo wamsaliti, vipi sasa wamtamani shemejio, sikio la kufa halisikii dawa."

Jamaa anamwambia rafiki yake kuwa kitendo anachokifanya ni cha aibu na kashfa ya hali ya juu. Kwa sababu anaelewa kabisa kuwa yule mwanamke ni mke wa rafiki yake kipenzi, lakini anamzunguka. Anamng'ong'a kisogo. Je sasa siku akija kujua itakuwaje?

Fikiria akafahamu kuwa kumbe siku zote hizi ambazo yeye hajui lolote, jamaa anamchukua mkewe? Siku zote hizi kumbe anafanywa mjinga? Tena afadhali kwa mtu ambaye labda hajui kama mwanamke yule ameolewa, lakini ni rafiki yake na anajua kuwa ni wanandoa, lakini anafanya mambo ya ajabu. Pata picha mtu huyo anaweza kuchukua hatua gani?

Upande wa pili, wako pia wanawake wenye tabia kama hiyo kama walivyoimba Msondo Ngoma, wakati huo ikiwa JUWATA Jazz, katikati ya miaka ya 1980. Nyimbo zote hizi mbili zilitungwa na mwanamuziki mahiri kwa utunzi kuwahi kutokea kwenye bendi hiyo, TX Moshi William.

Wimbo huu unaitwa 'Siwema', unaomsimulia mwanadada huyo aliyetumia ukaribu wake na mume wa rafiki yake kumlaghai mpaka akachukuliwa yeye na mwenzake kuachika.

"Tamaa yako dada itakuponza Siwema, umeweka tamaa nyingi Siwema dada nashangaa. Rafiki Neema kakasirika kwa kitendo ulichotenda kwa mumewe. Kumwita shemeji mara bwana. Neema alikuamini ukatumia mbinu zako, ukavunja ndoa yake. Siwema dada umemponza mwenzio, kaachika kwa mumewe kwa tamaa yako we

ushemeji ulizidi, nyumba ni Neema, ilikuwa nia yako, kutaka vunja ndoa yake dada, hehehe, leo tumekuona Siwema dada, hohoho Siwema dada ee.

Neema alikuamini kama rafiki mpenzi ee, juu yako na mumewe, ukatumia kila hila kumlaghai mumewe, tamaa yako dada imevunja mapenzi yake."

Huu nao ni mkasa mwingine ambao dada mmoja ni kama anamsuta Siwema kwa kitendo hicho alichofanya. Neema alidhani utani wa shoga yake Siwema ni ule wa mtu na shemeji yake, kumbe shoga yake alikuwa anautumia mwanya huo kumtega jamaa kama watoto wa sasa wanavyosema.

Jamaa akategeka kweli. Mchovya asali hachovyi mara moja. Na anayelamba asali, atachonga mzinga. Jamaa akamtimua kwa kumpa talaka mkewe kwani aliona ni kama vile anambanabana asitanue na 'ngoma yake mpya'.

Huu ni ukatili wa hali ya juu. Sasa kwa sisi binadamu huwezi kujua kama Neema ameondoka kwenda kwao huku akimuachia Mungu, au kuna kitu anaweza kukifanya kwa ajili ya kulipa kisasi. Tabu wakati mwingine ndiyo inaanzia hapo.

***Tuma meseji 0716 350534***

HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-10

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

HAKUTAKA kuelezea lolote lile lililotokea. Kila kitu kilibaki ni siri yake. Hata wazazi wake ambao walitaka kuuliza ilikuwaje akafanya kitendo kile, jibu lake lilikuwa moja tu.

"Nyinyi niacheni tu. Sina hata hamu ya kujibu hilo."

Wazazi wakaamua wakamuacha. Wakampokea kwa sababu ni binti yao. Watamtupia nani? Tikiti baya shambani mwako. Ingawa aliwatia aibu ya mwaka, lakini watafanyaje?

Kingine ambacho kilifanya wasimsakame sana binti yao ni kutopata upinzani kutoka kwa Jerry na familia yake. Walilia. Wakahuzunika, wakaondoka. Kikubwa zaidi hadi leo hii Jerry amekuwa kama ndugu yao. Amekuwa akifika kijijini hapo kwa mambo mbalimbali. Mara ya mwisho akimchukua Zulfa kwa ajili ya kumtibia, akigharamia kila kitu. Na akakaa na binti yao miezi miwili. Mwisho cha muhimu zaidi wakajua labda mambo yanaweza kumalizwa kidiplomasia na Vayajo akachukuliwa na Jerry. Ni kwa sababu amerudi nyumbani na pia bado wana mahusiano mazuri na muoaji.

Vayajo alikuwa anafahamu kila kitu kilichokuwa kikitendeka kwao tangu aondoke. Alikuwa anazipata habari kutoka kwa rafiki yake Nasma, au Naa kama ambavyo kijijini hapo walikuwa wanapendelea kumwita.

Alipotoroka alibadilisha namba ya simu. Lakini mara chache alikuwa akiirudisha ile namba ya awali, anampigia Naa na kumuulizia habari za kijijini hapo na nyumbani kwao, akiridhika, anag'oa laini na kuirudishia ile mpya. Ya zamani haipatikani tena.

Taarifa za ndugu yake kuumwa na nyoka, kulazwa pia alikuwa nazo ingawa hakuja. Taarifa za kuchukuliwa na kukaa kwa aliyemkimbia kabla ya ndoa pia zilikuwa mikononi mwake.

****************************

"Vipi da' Vayajo mbona umesimama hapa peke yako?" Akauliza Zulfa aliyekuwa anatoka kisimani na ndoo ya maji kichwani.

Njiani alimkuta dada yake akiwa amesimama peke yake karibu na kichaka.

Hakujibu kwa nusu dakika. Lakini sura na macho yake yalionyesha mashaka, au kuna kitu kinamsumbua.

"Dada vipi? Kuna nini?" Akauliza tena.

"Yaani Zulfa unajua ninavyokuchukia mbwa wewe?" Ni jibu ambalo hakutegemea. Na hakuna hata siku moja ambayo amewahi kukwaruzana na dada yake akamwambia maneno hayo. Jibu hilo lilimshtua sana. Kwanza




**"Unajitia kimbelembele kunifuatilia mambo yangu eee? Wewe bado mtoto mdogo sana kwangu. Umezaliwa nakuona, mimi wakati unazaliwa nimeshaanza kuwa na akili, leo unisumbue mtoto mdogo kama wewe? Bado Zulfa alikuwa kama yupo ndotoni**

alidhani huenda dada yake hayupo sawa. Au kuna kitu kisicho cha kawaida kimemkumba.

"Mmmh, dada uko sawa kweli?"

"Kwani umeniona nimepinda?" Akajibu, halafu akaendelea.

"Wewe bado mtoto mdogo sana kwangu."

"Kwani da' Vayajo nimefanya nini, mbona mimi sielewi kosa langu? Si nimerudi jana tu, tena hata hatujaongea sana, kuna nini umesikia maana hiki kijiji!"

"Hakuna kijiji wala wilaya, nasema hivi, nakuchukia Zulfa. Unajua kuchukia? Nakuchukia nakuchukia."

Zulfa na yeye kwa mbali moyo ulianza kumuenda mbio na hasira kuanza kumjia. Lakini alijitahidi kuzidhibiti.

"Nashukuru kwa kunichukia dada, lakini mimi kosa langu silijui." Akajibu. Kwa nje ilionekana kama amejibu kawaida, lakini ni jibu lililojaa hasira ndani yake.

"Unajitia kimbelembele kunifuatilia mambo yangu eee? Wewe bado mtoto mdogo sana kwangu. Umezaliwa nakuona, mimi wakati unazaliwa nimeshaanza kuwa na akili, leo unisumbue mtoto mdogo kama wewe?

Bado Zulfa alikuwa kama yupo ndotoni anaota. Ni kweli yule ni dada yake Vayajo au mwingine? Wakati akiendelea kumtafakari na kushangaa, dada yake alizidi kumporomoshea maneno.

"Unajifanya wewe ni mzuri. Una uzuri gani wa kunizidi mimi, mimi mzuri, hebu niangalie kwanza kuanzia mbele hadi nyuma, juu hadi chini. Nashangaa kujifanya malkia wakati huna lolote."

"He dada mbona mimi sikuelewi? Unanichukia mimi kwa sababu wewe mzuri mimi mbaya, au kwa sababu gani? Maana hapa nashindwa hata kukuelewa."

"Utanielewa tu mwaka huu Zulfa, yaani umenikera."

"Dada, mimi nakuheshimu, hebu funguka nikuelewe na mimi nijibu kile ambacho naona hakiko sawa, maana unaongea tu mwanzo hadi mwisho." Akajibu Zulfa akionekana maneno yameshaanza kumchosha.

"We Zulfa, siyo kila nikiongea unapenda kupanua domo lako, sipendi, mimi ni dada yako hata ufanye nini masikio hayazidi kichwa." Maneno hayo yalifuatiwa na singi. Kidole cha Vayajo kilisukuma kichwa cha Zulfa. Akayumba. Akajitengeneza balansi ili ndoo yake iliyokuwa imejaa maji isianguke.

Hakufanikiwa, kwani Vayajo alimsukuma kwa kutumia mwili wake, mdogo wake akaanguka na maji yakamwagika.

"Haya kamwambie mama yako." Vayajo akatamka kwa kejeli, huku mdogo wake akiwa chini akijizoazoa. Alionekana kuridhika na alichofanya, akageuka na kuondoka, huku akifyonya.

Akamuacha Zulfa akiangua kilio. Alilia kwa sauti kiasi cha dakika tano. Akalia kimya kimya kama dakika tatu hivi. Hakuna mtu yoyote aliyepita kwenye njia hiyo. Akajifikiria. Akawaza na kuwazua. Alinyanyuka kama mtoto yatima. Akakamua khanga yake aliyokuwa amevaa juu ya gauni. Ngata yake pia ililoa, akaikamua pamoja na gauni lake. Aliwaza arudi nyumbani au arejee tena kisimani kuchota maji mengine. Akaamua kurejea kisimani kuchota maji.

Alirejea majira ya saa 12;00 jioni akiwa hoi. Mama yake alipomtazama tu kwa mbali alivyokuwa akirudi aligundua hayupo sawa. Alipokaribia, aligundua pia nguo zake zilikuwa zimeloana.

Kando ya mama yake Vayajo alikuwa amejaa tele kama pishi la mchele. Zulfa alimuona vizuri dada yake aliyekuwa amepeleka kidole chake mdomoni. Ilikuwa ni ishara aliyoifahamu vema. Ya kwamba afunge mdomo wake. Ina maana asimwambie lolote mama yao.

"Vipi mwenzetu mbona hivyo?"

Hakujibu kitu, alikwenda ndani kutua ndoo. Akabaki ndani kwa dakika 10 hivi. Alipotoka alikuwa amebadilisha nguo.

"Enhe mwenzetu kimekupata nini mbona hivyo?"

"Nilianguka." Akajibu kifupi kwa haraka.

"Wapi?" Mama akauliza tena.

"Njiani wakati narudi na maji, ikabidi nirudi tena nikachote." Akazidi kumdanganya mama yake.

"We nawe umezidi kutembea kama bata, ndiyo maana huwa unaangukaanguka."

Wakati huo pembeni, Vayajo alikuwa anakauka kwa kucheka, ingawa kimya kimya bila kutoa sauti.

Mama aligeuka ghafla kama kuna kitu alitaka kumwambia Vayajo. Alichokutana nacho ni kicheko cha kimya kutoka kwake.

"Na wewe kinachokuchekesha nini? Mwenzako kaanguka wewe unacheka badala ya kumpa pole."

"Mimi nimecheka hilo neno la kuwa anatembea kama bata." Vayajo naye alidanganya.

ITAENDELEA JUMAPILI

# RHODA ATAMANI UWANAMITINDO KIMATAIFA



Na Halfani Chusi

MWANAMITINDO anayekuja kwa kasi, Rhoda Kipingo amesema fani hiyo sawa na ajira zingine na kwamba lengo lake ni kuja kuwa wa kimataifa.

Rhoda aliliambia Nipashe, baada ya kupita katika magumu , kwa sasa ameanza kupata mafanikio kutokana na kipato kikubwa anachopata.

Amesema anatamani siku moja kuacha alama katika taifa kwa kuwasaidia wengine kutokana na wengi kutoka katika familia masikini kama yeye.

"Licha ya kwamba najishughulisha na ujasiriamali wa kuuza vifaa mbalimbali vya simu, na kufanya huduma za kifedha lakini uwanamitindo ndio ndoto yangu kubwa. Watu wengi huwa wanakuja na kuomba ushauri kwangu watokaje kwenye sherehe zao,"

Amesema ameanza kufungua ofisi yake inayojishughulisha na mitindo eneo la Kigamboni ili kuwa karibu na watu.

"Licha ya kupenda mitindo pia nina biashara ya kuuza simu na vifaa vyake, ninaamini kwenye kujituma na kufanya kazi kwa bidii" ameongeza kusema.

Rhoda, mabaye ni muhitimu wa chuo cha ualimu na mama wa mtoto mmoja, amewasihi wahitimu wenzie kutobweteka na badala yake watumie fursa kujiajiri.

## Rose Shaboka kuipamba'limbwata'



Mchungaji mrembo anayetikisa mitandao ya kijamii kwa mafundisho yake ya ndoa na mahusiano, Pastor Rose Shaboka, atatambulisha kitabu chake cha Limbwata kwa burudani kabambe.

Akizungumza na Nipashe jana, mchungaji Rose amesema kitabu hicho kitatoka Desemba 30, mwaka huu na ni zawadi yake kwa wanawake wote walioko kwenye ndoa au mahusiano.

"Ni kitabu nilichokiandika nikitumia uzoefu wangu mwenyewe kama mke, mchungaji na mshauri ambaye nakutana na kesi nyingi za ndoa lakini pia kwa kufanya utafiti na kuchukua maoni kutoka kwa wanaume wenyewe na wale wenye ndoa zilizofanikiwa kudumu kwa muda mrefu," amesema Rose Shaboka.

Aliongeza kuwa kuanzia sasa watu wote wanaweza kuweka oda kabla hakijatoka kwa bei ya 10,000 pekee kwa kuwasiliana naye kwenye mitandao yake ya kijamii au 0765190462 na ofa hiyo itaisha Desemba 27 na baada ya hapo bei itabadilika.

## ZISIKUPITE

### GRIEZMANN ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United inafikiria kumuwania, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 31 kutoka Atletico Madrid. (***Mediafoot***)

### MADRID WAJITOSA KWA GAKPO

REAL Madrid imejiunga katika mbio za kuwania kumsajili mchezaji mwenye umri wa miaka 23 wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo anayehusishwa na Manchester United na Newcastle. (***Mirror***)

### CODY KUMRITHI RONALDO

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili Cody Gakpo aliyefunga mabao matatu katika kombe la dunia 2022, ifikapo Januari akitarajiwa kuchukua nafasi ya Cristiano Ronaldo. (***Telegraph***)

### ISCO ATAKIWA WOLVES

KLABU ya Wolves inajaribu kumsajili mshindi mara tano wa ligi ya mabingwa Ulaya, Isco kutoka Sevilla. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 30 aliyekuwa akicheza nafasi ya kiungo wa kati kule Real Madrid pia anasakwa na Juventus, Napoli na Aston Villa. (***Todofichajes***)

### WOLVES KUSAJILI SITA

HUENDA ikawa Januari yenye shughuli nyingi za uhamisho kwa klabu ya Wolves inayotaka kuwasajili hadi wachezaji sita wapya wakati dirisha la uhamisho litafunguliwa. Kocha Julen Lopetegui ameashiria anataka kuongeza wachezaji zaidi kutoka kikosi hicho. (***Times***)

### KUDUS NA EVERTON

KLABU ya Everton itajiunga katika kumuwania kumsajili mchezaji wa Ajax mwenye umri wa miaka 22 raia wa Ghana, Mohammed Kudus katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Ekrem Konur kwenye Twitter***)

### RABIOT AITAKA BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Juventus na timu ya taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 27 ameelezea matamanio yake ya kujiunga na Barcelona. (***Sport***)

### RONALDO KUSTAAFU SOKA

CRISTIANO Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 huenda anajitayarisha kutangaza kustaafu, amesema Patrice Evra aliyewahi kucheza na mshambuliaji huyo wa Ureno katika klabu ya Manchester United. Ronaldo hajasajiliwa katika klabu yoyote baada ya kuondoka United Novemba. (***Sky Sports***)

### BELLINGHAM AWINDWA

NEWCASTLE United, Middlesbrough na Sunderland zote zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Birmingham City, Jobe Bellingham mwenye mwenye umri wa miaka 17. (***Teamtalk***)

### OUNAHI AGOMBEWA NA KLABU

LEICESTER, Wolves na West Ham ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mchezaji wa Morocco mwenye umri wa miaka 22, Azzedine Ounahi baada ya kuwavutia katika kombe la dunia. Ounahi anaichezea Angers inayoshiriki Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1. (***Sky Sports***)

### MBAPPE MDOGO AANZA PSG

ETHAN Mbappe ambaye ni mdogo wake na Kylian mwenye umri wa miaka 15, alianza kuichezea Paris St-Germain katika mechi ya kirafiki dhidi ya Paris FC na kushinda 2-1 Ijumaa. (***Athletic***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# INFANTINO: KOMBE LA DUNIA 2022 LIMEKUWA BORA ZAIDI

## ●●● Sasa Fifa yajipanga kwa michuano ya 2026, huku timu zikiongezwa hadi 48...

**DOHA,** Qatar

RAIS wa Shirikisho la soka la kimataifa, FIFA, Gianni Infantino amesema Kombe la Dunia la mwaka huu linalomalizika leo nchini Qatar ni bora zaidi katika historia ya mashindano hayo.

**Infantino alikuwa akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari nchini Qatar, baada ya kuhudhuria mkutano wa baraza la Fifa.**

Alisema kuwa mashabiki milioni 3.27 ndio waliohudhuria kwenye mechi ikilinganishwa na mashabiki milioni 3.3 waliohudhuria katika Kombe la dunia la Urusi mwaka 2018.

"Asante kwa kila mmoja aliyehusika, Qatar, wale wote waliojitolea kulifanya Kombe hili la Dunia kuwa bora zaidi kuwahi kushuhudiwa," alisema Infantino.

"Mechi zimechezwa bila matukio. Kumekuwa na hali ya furaha sana.'

"Kuna kitu kinachotokea tunapozungumzia kuhusu soka kuwa mchezo halisi wa dunia, huku timu ya Afrika (Morocco) ikifika nusu fainali kwa mara ya kwanza."

Wakati huo huo rais huyo wa Fifa amesema shirikisho hilo litaangalia upya mpangilio wake katika Kombe la Dunia la 2026 litakalofanyika kwa ushirikiano wa nchi tatu Marekani, Mexico na Canada.

Timu zitaongezeka kutoka 32 hadi 48 kwa ajili ya shindano hilo, na zinapangwa kugawanywa katika makundi 16 ya timu tatu, ambapo timu mbili zitakazoongoza katika kila kundi zitaendelea na kuingia katika hatua ya 32.

Infantino amesema kwamba hilo litaangaliwa baada ya "mafanikio" ya makundi ya timu nne katika Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
ARGENTINA
VERSUS
FRANCE
1 | 2.70
X | 3.05
2 | 2.70

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VAN DIJK KUKOSA MECHI YA MAN CITY




**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amependekeza hatafikiria kumchezesha Virgil van Dijk wakati Liverpool itakapovaana na Manchester City wiki ijayo kwenye mchezo wa kombe la Ligi (EFL), Desemba 22.

Van Dijk alirejea mazoezini na Liverpool huko Dubai wiki hii baada ya Uholanzi kuondolewa kwenye Kombe la Dunia dhidi ya Argentina Ijumaa iliyopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alishiriki kikamilifu katika mechi zote tano za nchi yake nchini Qatar - ikiwa ni pamoja na muda wa ziada wakati wakipoteza kwenye robo fainali dhidi ya Argentina - akicheza jumla ya dakika 480.

Hata hivyo, wakati Klopp hataki kuharakisha kurejea kwa Van Dijk, bado hajawapigia simu wachezaji wawili wa England, Jordan Henderson na Trent Alexander-Arnold.

Henderson hakumaliza mechi yoyote kati ya tatu za England alizoanza, huku Alexander-Arnold akicheza kwa dakika 33 tu uwanjani katika mechi tano za Simba Watatu hao. "Ndiyo, kuna nafasi, bila shaka - wanafanya mazoezi tayari," alisema. Klopp aliiambia tovuti rasmi ya Liverpool alipoulizwa kama kuna wachezaji watakaorejea kwenye Kombe la Dunia watakaocheza dhidi ya City.

"Hendo tayari anafanya mazoezi hapa, Virgil anafanya mazoezi hapa, lakini sidhani kama tutajaribu. Hendo tutaona, Trent tutaona.

"Lakini kikundi hiki kilifanya kazi pamoja kwa karibu wiki mbili na tulipiga hatua ya kweli na hiyo ni nzuri. Sijui kwa wakati huu.

"Natumai sote tutaimaliza na sote tunajua huko England, na huko Ulaya kwa ujumla, kuna aina ya virusi vinavyozunguka, kwa hivyo tunatumaini kuwa tunaweza kujiepusha na hilo.

"Basi tutafanya uamuzi ni wazi Jumatano nani anaweza kucheza Alhamisi. Lakini ni mzuri na utakuwa mchezo wa kuvutia sana baada ya kipindi hicho, lakini ninausubiri kwa hamu."

Liverpool iliifunga AC Milan 4-1 katika mechi yao ya pili ya kirafiki katikati ya msimu siku ya Ijumaa, huku Darwin Nunez akifunga mara mbili.

Baada ya safari ya Liverpool kwenye Uwanja wa Etihad, siku nne baadaye watakwenda Aston Villa kwenye mechi za Ligi Kuu kabla ya kuwakaribisha Leicester City Desemba 30.

# Benzema akataa kujiunga na Ufaransa




**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema aliingia kwenye mitandao ya kijamii na ujumbe wa siri akisema "sivutiwi" siku mbili tu kabla ya mchuano wa fainali ya Kombe la Dunia kati ya Ufaransa na Argentina.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid, Benzema aliachwa kwenye safari ya Qatar usiku wa kuamkia kuanza kwa michuano hiyo kutokana na jeraha la paja.

Kulikuwa na maoni kwamba mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or anaweza kuunganishwa na kikosi baada ya kupona jeraha na kurejea kwenye timu ya taifa.

Hata hivyo, alipoulizwa kama Benzema anaweza kurejea kabla ya fainali ya leo Jumapili, bosi wa Ufaransa, Didier Deschamps alijibu: "Sitaki kukujibu. Ni swali la kijinga."

Ripoti zaidi kutoka Hispania zilidai Benzema hakufurahishwa kurudishwa nyumbani mara ya kwanza na hakukubali mpango wa Deschamps kumjumuisha kwenye fainali.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alichapisha ujumbe wenye utata kwenye mitandao ya kijamii, uliotafsiriwa tu kama "Sivutiwi".

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Lyon, amefunga mabao 37 katika mechi 97 alizoichezea Ufaransa.

## HABARI MICHEZO

Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# MABONDIA 10 FITI KUELEKEA USIKU WA MABINGWA ARUSHA

**Na Saada Akida**

JUMLA ya mabondia 10 jana wamefanikiwa kupima afya tayari kwa maandalizi ya mwisho kuelekea pambano la usiku wa mabingwa linalotarajiwa kufanyika Desemba 26, mwaka huu katika ukumbi wa AICC lake Nyasa, Arusha.

Mabondia hao ni Hamad Furahisha, Zawadi Kutaka, Hassan Ndonga, Haidary Mchanjo, Halima Vunja Bei, Sylvester Urio, Karim Mandonga, Ramadhani Kumbele, Iddi Pialali na Mfaume Mfaume.

Mabondia hao watacheza pambano hilo akiwemo Mfaume wa Mabibo ambaye anatarajia kucheza pambano kuu dhidi ya Pialali kutoka Manzese, Dar es Salaam huku kiingilio kikubwa katika pambano hilo kikiwa ni Sh 50,000.

Mratibu wa pambano hilo, Bakari Khatibu alisema kuwa wamekamilisha zoezi la kwanza kwa upimaji afya za mabondia kuelekea kwenye pambano hilo ambalo linasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa mchezo huo.

"Tayari leo (jana), waandaaji tumekamilisha sehemu ya kwanza ya maandalizi kwa kuwapima afya mabondia wote kutokana na kanuni na sheria za mchezo wa ngumi za kulipwa hapa nchini," alisema.

"Kitu kikubwa ambacho tunataka kuwaambia mashabiki tukiwa kama waandaji tumekuwa tukifanya mambo kwa utofauti mkubwa katika jiji la Arusha kwa kuwapelekea burudani ya masumbwi usiku wa mabingwa kati ya Mfaume na Piarali," aliongeza Khatibu.

Miongoni mwa mabondia waliopima afya ni Mandonga ambaye amewataka mashabiki wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi katika usiku wa mabingwa huku akisisitiza kuwepo kwa ngumi yake ya akishinda Oya oya na akipigwa oya oya kwenye pambano hilo.

Kwa upande wa daktari aliyesimamia zoezi hilo, Khadija Hamisi alisema kawaida wamekuwa wakisimamia kuwapima magonjwa matatu kabla ya kupanda ulingoni ambapo aliyataja magonjwa hayo ni homa ya ini, kisukari na ukimwi.



Wachezaji wa timu ya mpira wa Kikapu ya Vijana wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ni Fainali ya kisasi kombe la dunia leo

INATOKA UK. 24

Kwa hakika, Les Bleus wameshinda mechi saba za mtoano za Kombe la Dunia mfululizo - mbili nyuma ya rekodi ya Brazil - huku wakitarajia kuwa timu ya tatu tu (baada ya Brazil 1962 na Italia 1938) kutetea taji la kombe la Dunia.

Golikipa wa Ufaransa, Hugo Lloris anaweza kuwa mchezaji wa kwanza kuwa nahodha wa timu kushinda katika fainali mbili mfululizo za kombe la dunia.

Na Deschamps anaweza kuwa kocha wa kwanza kutetea taji la kombe la dunia baada ya Vittorio Pozzo alipofanya hivyo akiwa na Italia katika miaka ya 1930.

## Simba SC yaanza kusaka pointi tisa Kanda ya Ziwa

INATOKA UK. 24

Alisema malengo yao ni kuhakikisha duru la pili wanapambana kila mechi na kuvuna pointi tatu na leo Jumapili wakianza na Geita Gold.

Katika hatua nyingine Ahmed amewataka mashabiki kuwa na uvumilivu katika suala zima la usajili huku viongozi wakiendelea na mchakato wa kuleta wachezaji wapya wa kuongeza nguvu kikosini.

"Tayari uongozi umeshaanza kufanyia kazi mapendekezo ya usajili, kuna ambao tayari tumeshamalizana nao na wengine mazungumzo yanaendelea, kuhusu nani na nani ikifika muda tutaweka hadharani," alisema Ahmed.

Alisema kuhusu staili yao ya utambulisho msimu huu watakuja kivingine hasa kulingana na usajili ambao wanaufanya.



## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 18/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4764 | Real Betis B vs Antequera CF | 2.68 | 2.83 | 2.68 |
| 13:30 | 5695 | Melilla vs AD Alcorcon B | 1.33 | 4.28 | 8.57 |
| 14:00 | 1768 | Lleida Esportiu vs Llagostera | 2.16 | 2.96 | 3.34 |
| 14:00 | 1901 | CD Badajoz vs CD Linares | 2.11 | 3.01 | 3.40 |
| 14:00 | 1956 | CA Osasuna B vs CE Sabadell | 1.99 | 3.06 | 3.69 |
| 14:00 | 2179 | CF Algeciras vs Pontevedra | 1.99 | 3.07 | 3.70 |
| 14:00 | 2334 | Velez CF vs Sevilla Atletico | 2.02 | 3.21 | 3.40 |
| 14:00 | 2463 | CD Eldense vs CD Calahorra | 1.65 | 3.45 | 4.86 |
| 14:00 | 2632 | Fuenlabrada vs Real Madrid Castilla | 3.31 | 3.02 | 2.14 |
| 14:00 | 2672 | Yeclano Deportivo vs Granada B | 1.85 | 3.32 | 3.86 |
| 14:00 | 3107 | Athletic Bilbao B vs SD Logrones | 2.28 | 3.05 | 3.00 |
| 14:00 | 3608 | CE Manresa vs Espanyol B | 2.44 | 3.03 | 2.78 |
| 14:00 | 3679 | Olot vs Mallorca B | 2.22 | 2.88 | 3.32 |
| 14:00 | 3686 | Mbeya City vs Dodoma FC | 1.73 | 3.25 | 5.40 |
| 14:00 | 3721 | CD Laredo vs SD Compostela | 3.01 | 2.96 | 2.32 |
| 14:00 | 4445 | CF Villanovense vs UD Montijo | 2.04 | 3.06 | 3.54 |
| 14:00 | 4480 | AD Ceuta vs Deportivo La Coruna | 4.36 | 3.39 | 1.74 |
| 14:00 | 4580 | SC Huelva W vs Tenerife Sur W | 2.48 | 3.31 | 2.53 |
| 14:00 | 4646 | Real Oviedo B vs Coruxo | 2.73 | 2.88 | 2.59 |
| 14:00 | 4741 | Ucam Murcia vs FC Cartagena II | 1.84 | 3.26 | 3.99 |
| 14:00 | 5015 | Real Aviles vs UP Langreo | 1.62 | 3.53 | 5.04 |
| 14:00 | 5220 | Kocaelispor vs Ankara Demirspor | 1.71 | 3.75 | 4.60 |
| 14:00 | 5594 | Atletico Baleares vs Real Murcia | 2.44 | 2.88 | 2.92 |
| 14:00 | 5662 | Unionistas CF vs Celta B | 2.15 | 3.05 | 3.25 |
| 14:30 | 2009 | Catanzaro vs Potenza SC | 1.47 | 4.40 | 6.19 |
| 14:30 | 2520 | Messina FC vs Taranto Sport | 2.26 | 3.09 | 3.29 |
| 14:30 | 3052 | Pescara Calcio vs AZ Picerno | 1.66 | 3.61 | 5.21 |
| 14:30 | 3606 | Atletico Sanluqueno vs Cadiz B | 1.85 | 3.22 | 4.00 |
| 14:30 | 5299 | Torre Neapolis vs Foggia | 3.19 | 3.19 | 2.25 |
| 14:30 | 5526 | FC Giugliano 1928 vs Crotone | 3.54 | 3.19 | 2.11 |
| 14:30 | 5696 | Luton Town vs Millwall | 2.46 | 3.02 | 2.92 |
| 15:00 | 5783 | Kariobangi Sharks vs Gor Mahia | 3.55 | 2.97 | 2.07 |
| 15:30 | 5733 | Petrolul Ploiesti vs U Craiova SA | 2.84 | 2.99 | 2.54 |
| 15:45 | 2102 | AE Larissa vs PO Triglias | 1.66 | 3.35 | 5.04 |
| 15:45 | 2940 | Proodeftiki FC vs Irodotos | 1.43 | 3.85 | 7.02 |
| 15:45 | 3087 | Iraklis Larisas vs Niki Volou | 16.65 | 5.09 | 1.19 |
| 16:00 | 1041 | Cosenza vs Ascoli | 2.67 | 2.96 | 2.72 |
| 16:00 | 1682 | Geita Gold FC vs Simba | 3.76 | 2.19 | 1.55 |
| 16:00 | 2506 | Parma vs Spal | 1.67 | 3.57 | 4.95 |
| 16:00 | 3404 | Modena vs Benevento | 2.43 | 3.07 | 2.92 |
| 16:00 | 4455 | Ternana vs Como | 2.00 | 3.32 | 3.57 |
| 16:00 | 5014 | Albacete Balompie vs UD Ibiza Eivissa | 1.82 | 3.32 | 4.36 |
| 16:00 | 5787 | Cittadella vs Sudtirol | 2.02 | 3.03 | 3.92 |
| 18:00 | 1927 | Argentina vs France | 2.70 | 3.05 | 2.70 |
| 20:45 | 2982 | Palermo vs Cagliari | 2.68 | 3.07 | 2.63 |
| 21:00 | 1625 | Burgos vs Huesca | 2.32 | 2.88 | 3.32 |
| 21:00 | 5974 | Levante vs Eibar | 2.09 | 3.12 | 3.56 |
| 21:30 | 1476 | UTA Arad vs Rapid Bucuresti | 3.12 | 3.02 | 2.34 |
| 22:45 | 2462 | Genoa vs Frosinone | 2.00 | 3.12 | 3.86 |
| 23:00 | 1205 | Malaga vs Alaves | 2.87 | 2.92 | 2.57 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Desemba 18, 2022

Nipashe



Infantino: Kombe la Dunia 2022 bora zaidi UKURASA 21

# NI FAINALI YA KISASI KOMBE LA DUNIA LEO

## Argentina ikiivaa Ufaransa, rekodi yatoa taswira nani kuibuka mshindi, ni vita ya Messi na Mbappe...




**DOHA, Qatar**

FAINALI ya kombe la Dunia leo Jumapili itakuwa ni mara ya 13 kwa Argentina kukutana na Ufaransa katika soka la kimataifa la wanaume.

Ufaransa wameshinda mechi tatu pekee kati ya 12 za awali, huku Argentina wakiwa wameshinda mara sita.

Mchezo wa leo Jumapili unaonekana kwa wengi kama pambano kati ya Kylian Mbappe na Lionel Messi.

Wanaume wote wawili waling'ara mara ya mwisho Ufaransa ilipocheza na Argentina katika Kombe la Dunia.

Mbappe alifunga mara mbili naye Messi akaandikisha pasi mbili za mabao Ufaransa ilipoichapa Argentina 4-3 katika hatua ya 16 bora nchini Urusi miaka minne iliyopita.

Messi alikuwa kwenye orodha ya mabao miaka tisa mapema mwaka wa 2009 - mara ya mwisho kwa Argentina kuishinda Ufaransa.

Ufaransa ilishinda 4-3 mwaka 2018, lakini Argentina wana rekodi ya juu zaidi ya uso kwa uso katika mikutano yao yote 12 kabla ya leo.

Messi hii itakuwa ni mechi yake ya mwisho ya Kombe la Dunia na ataweka rekodi ya kucheza mechi 26, kwani ameshatangaza wazi kwamba hataichezea tena Argentina.

Nahodha huyo wa Argentina alikuwa sehemu ya timu iliyofungwa 1-0 na Ujerumani katika fainali ya kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil.

Kwenye michuano ya mwaka 2018 nchini Urusi waliishia hatua ya 16 bora baada ya kufungwa na Ufaransa.

Messi amekiongoza kikosi chake kutimua vumbi kwenye Uwanja wa Lusail wakati huu, ambapo Ufaransa ni wapinzani wao tena.

Ushindi wa Ufaransa dhidi ya Argentina sio mzuri kiasi hicho, kwani wameshinda mechi tatu pekee kati ya 12 dhidi yao katika mashindano yote na kupoteza mechi mbili kati ya tatu za Kombe la Dunia, lakini ushindi wao mkubwa ni wa 4-3 kwenye Kombe la Dunia lililopita wakiwa chini ya kocha wa sasa, Didier Deschamps.

INAENDELEA UK. 23

# Simba SC yaanza kusaka pointi tisa Kanda ya Ziwa

**Na Saada Akida**

WEKUNDU wa Msimbazi, Simba wamedhamiria kuhakikisha wanaondoka na pointi zote tisa katika mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara watakazocheza Kanda ya Ziwa kuanzia leo Jumapili.

Simba ipo Kanda ya Ziwa na leo Jumapili itacheza na Geita Gold kabla ya kuwavaa Kagera Sugar na baadae kucheza na KMC.

Mechi hizo zote Simba itacheza ugenini katika Kanda ya Ziwa ambapo timu hizo zinatumia viwanja vya huko.

Simba wanaoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara wako nyuma ya vinara Yanga kwa pointi nne hivyo wanahitaji pointi tisa ili kuongeza mbio za kuwania taji hilo msimu huu wa 2022/23.

Akizungumza na gazeti hili, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally amesema maandalizi yanaendelea vizuri na kikosi chao kipo jijini Mwanza kikiwa na wachezaji wote wakiwa fiti kasoro Peter Banda ambaye ni majeruhi.

"Wachezaji wote wako fiti na wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi zetu za Kanda ya Ziwa tunaenda kupambana kutafuta pointi tatu kila mechi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya mbio za ubingwa," alisema Ahmed.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >